

MASWALI YA USHAIRI

Kwa Majibu,wasiliana naye sir ABRAHAM **0729125181**



Strive for progress

The following materials are also available;

- 👉 High school topical questions
- 👉 Primary topical questions
- 👉 High school summarised notes
- 👉 KCSE & KCPE predictions
- 👉 Termly exams
- 👉 Updated schemes of work
- 👉 Highschool mocks and pre-mocks
- 👉 KCPE & KCSE past papers
- 👉 Setbook questions and guides

N/b, all questions are free but notes and set guides incl

welcome for topflight publishers products



Call/text/WhatsApp Sir Abraham@0729125181

O C Bilingual



Edit with WPS Office

1. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

KIPIMO NI KIPI?

1. Nitampa nani, sauti yangu ya dhati,
Kwa kipimo gani, ingawa kiwe katiti,
Ameanya nini, la kuleta umati,
Kipimo ni kipi?
2. Yupi wa maani, asosita katikati,
Alo na maoni, yasojua gatigati,
Atazame chini, kwa kila ule wakati,
Kipimo ni kipi?
3. Alo mazalendo, atambuaye shuruti
Asiye mafundo, asojua mangiriti
Anoshika pendo, hata katika mauti,
Kipimo ni kipi?
4. Kipimo ni kipi? Changu mimi kudhibiti,
Utu uko wapi, ni wapi unapoketi,
Nje kwa Mkwapi, au ndani kwa Buheti,
Kipimo ni kipi?

Maswali

- (a) Eleza umbo la shairi hili (alama 4)
- (b) Taja tamathali moja ya usemi na kuieleza kisha utoe mfano wake kutoka kwa shairi.(alama 3)
- (c) Mshairi ana uhuru wa uandishi anapotunga shairi. Taja na ueleze mifano yoyote ya matumizi ya uhuru huo kisha utolee mifano kabambe. (alama 5)
- (d) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari. (alama 4)
- (e) Eleza msamiati ufuatao kama ulivytumiwa katika ushairi. (alama 4)
 - (i) Katiti
 - (ii) Gatigati
 - (iii) Shuruti
 - (iv) Mangiriti

2. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

HAKI YANGU 'TAIDAI

1. Haki ya mtu thawabu, kudai sitasita,
Hata nipatishe tabu, muhali mumi kukita,
Kulitenda la wajibu, liwe hai au mata,
Nitafanya majaribu, na inapobidi matata,
Haki yangu 'taidai, hata iwe ni kwa vita.

2. Haki ya mtu u'ngwana, siseme mimi nateta,
Sitaukiri ubwana, na jeuri unoleta,
Na ikiwa ni kuwana, sitajali sitajuta,
Sikiri kuoneana, na kupakana mafuata
Haki yangu 'taidai, hata iwe ni kwa vita.

3. Haki ifukie chini, ipige na kuibuta,
Tumbukize baharini, 'tazamia kuifuata,
Ukaifiche jangwani,nitakwenda kuileta,
Hundike milimani,nitawana kuipata
Haki yangu 'taidai, hata iwe ni kwa vita.

4. Hati ijengee ngome, izungushie na kuta,
Na fususi isimame, iwe inapitapita,
Tainuka nishikame, haki yangu kukamata,
Sifa kubwa mwanamme, kwenenda huku wasota,
Haki yangu 'taidai, hata iwe ni kwa vita.

5. Uungwana siuuzi, kwa njugu au kashata,
Ahadi za upuuzi, na rai kuitaita,
Kwa kila alo maize, hawi mithili ya bata,
Tope yake makaazi, na chakula cha kunata,
Haki yangu 'taidai, hata iwe ni kwa vita.

Maswali

- (a) Toa kichwa kinachofaa shairi hili. (alama 1)

- (b) Eleza kwa ufupi maudhui ya shairi hili (alama 4) .
- (c) Eleza umbo la shairi hili. (alama 5)

- (d) Ni nini maana ya 'sikiri kuoneana na kupakana mafuta?' (alama 2)
- (e) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivotumika katika shairi. (alama 4)
(i) Muhali

- (ii) Mata
 - (iii) Kuibuta
 - (iv) Fususi
- (f) Mshairi ana uhuru wa kurefusha au kufupisha maneno ili kuleta urari wa mizani na vina.
- (i) Toa mfano wa mbinu ya kufupisha bila kutumia ritifaa (alama ya ung'ong'o)
- (al.4)

(ii) Toa mfano wa mbinu ya kurefusha. Mbinu hii yaitwaje?

3. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

UKUBWA JAA

1

Dunia yetu dunia, watu wanakuftini,
Dunia huna udhia, waja wanakulaani,
Dunia huna hatia, wabebeshwa kila *zani*,
Dunia unaonewa, umetenda kosa gani?

2

Dunia umenyamaza, umetua kwa makini,
Dunia vitu 'mejaza, watu wanataka nini?
Dunia wanakucheza, binadamu *maliuni*,
Dunia unonewa, umetenda kosa gani?

3

Dunia mtu akose, hukutia mdomoni,
Dunia hebu waase, hao watu mafatani,
Dunia chuki mpuse, muipate afueni,
Duni unaonewa, unatenda kosa gani?

4

Dunia una lawama, za uongo si yakini,
Dunia wanokusema, ni manjunju si razini,
Dunia huna hasama, waja ndio kisirani,
Dunia unaonewa, umetenda kosa gani?

5

Dunia kuharibika, hayo amezusha nani?
Dunia watu humaka, hao wano kuhini,
Dunia umejazika, kila tunu ya thamani,
Dunia unaonewa, umetenda kosa gani?

6

Dunia unatukisha, bwerere bila undani,
Dunia unatukosha, maji tele baharini,
Dunia unaotesha, mimea tosha shambani,
Dunia unaonewa, umetenda kosa gani?

7

Dunia huageuka, tangu umbwe na Manani,

Dunia watu ndo nyoka, mahaini na wahuni,
Dunia una baraka, mwenye pupa hazoni,
Dunia huna ubaya, wabaya ni insani.

Maswali

- (a) Shairi hili ni la bahari gani? Toa sababu kwa jibu lako. (alama2)
- (b) Eleza umbo la shairi hili. (alama 4)
- (c) Ni uhuru gani wa kishairi aliotumia mtunzi? (alama 4)
- (d) Eleza sifa tatu za wanadamu kama anavyoeleza mshairi. (alama 3)
- (e) Kwa kurejelea mifano kutoka shairi, taja mbinu mbili za lugha zilizotumiwa
- (f) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari.(alama 3)
- (g) Eleza maana ya maneno haya kama yalivytumika katika shairi. (alama 2)
 - i)zani
 - ii)Maliuni

4. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

NAZI VUTA N'KUVUTE

1

ANITA: Ndugu ulo mnazini, wanavitafuta balaa
Nakwambya, shuka tini, katakata wakataa
Wafanya ni masikani, mustarehe mekaa
Utashuka au la?

2

AKIDI: Ndugu tini ya manazi, nilo juu nakujibu
Haya ni ya upuuzi, elewa wako wajibu,
Kushuka tini siwezi, pasi kujuwa sababu
Hilo ndo langu jawabu

3

ANITA: Sababu ya kukuambiya, ya kwamba ushuke tini
Ni kuwa nataka kweya, huko juu mnazini
Kwa ajili nami piya, nitunde nazi mwendani
Nishakweleza kwa nini.

4

AKIDI: Hayo ni ya kutesha, unambiyayo ndu yangu
Wataka niteremsha, juu ya mnazi wangu?
Wanistaajabisha, kuniamuru kwa uchungu
Una kisha mwenzangu?

Maswali

- (a) Fafanua bahari tatu kuu za shairi hili. (alama 3)
- (b) Onyesha namna mshairi alivyofaulu katika kutumia uhuru wa kishairi katika utunzi huu. (alama 4)
- (b) Ni nini dhamira ya mwandishi wa shairi hili? (alama 3)
- (c) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari.(alama 4)
- (d) Fafanua maana ya “ una kisha mwenzangu?” (alama 2)
- (e) Kwa nini Anita anamtaka Akidi atoke mnazini? (alama 1) .
- (f) Toa maana ya maneno yafuatayo kama yalijotumika katika shairi (alama 3)
- i)Tini
 - ii)Mnazi
 - iii)Kisha

5. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

MKULIMA

1. Mtazameni.....nguo ya Afrika,
Mtumwa wa watumwa waloridhiya!
Amekita jembe lake akilisujudia,
Kwa tambo liloumbuka na kuselehea,
Uso ukifuka ukata ulojifanya tabia,
Na machungu ya maonevu alovumilia.
2. Moyo wake mzito ulokokomaa kama kuni,
Haujui tena kutarajia wala kutamani,
Umekufa ganzi, kutohisi raha wala huzuni.
3. Basi iteni fikira mambo mukiyafikiri,
Siku hamaki yake itapochafuka kama bahari,
Siku ukweli wa hali yake utapodhihiri,
Umejiandalia vipi kutuambiya nini,
Huo mkono ulomuumbua na kumkausha,
Hizo pumzi zilomzimia taa ya maisha,
Kumfunga kizuizi, gazini kumtowesha?
4. Ni jawabu gani alowekewa na wakati,
Kulipoza ghadhabu ya ku ingawa katiti,
Kuliwaza hamaki ya njaa hii ya dhati,

Njaa ya maisha itakayo kushibishwa.

Maswali

- (a) Taja mambo mujimu yanayojitokesha katika shairi hili. (alama 5)
- (b) Taja na utoe mifano ya aina zozote tatu za tamathali za semi zilizotumika katika shairi hili. (alama 3)
- (c) Eleza umbo la shairi hili. (alama 4)
- (d) Fafanua maana ya: (alama 2)
 - i)siku ya hamaki yake itakapochafuka
 - ii)kuipoza ghadhabuya kiu ikawa katiti
- (e) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivytumiwa katika shairi. (alama 3)
 - i)tambo
 - ii)ulokomaa
 - iii)kumtowesha

6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

1. Mkata ni mkatika, harithi hatorithiwa,
Sina ninaloshika, wala ninalochukuwa,
Mlimwengu kanipoka, hata tone la muruwa,
Mrithi nini wanangu?
2. Sina ng'ombe sina mbuzi, sina konde sina buwa,
Sina hata makaazi, mupasayo kuyajuwa,
Sina mazuri makazi, jinsi nilivyoachiwa,
Mrithi nini wanangu?
3. Sina kazi sina bazi, ila wingi wa shakawa,
Sina chembe ya majazi, mno ni kukamuliwa,
Nakwacheni upagazi, mgumu kwenu kutuwa,
Mrithi nini wanangu?
4. Sina sikuacha jina, mkata hatasifika,
Hata nifanye la mana, mno ni kulaumiwa,
Poleni wanangu, sina kwenu cha kutowa,
Mrithi nini wanangu?

5. Sina leo sina jana, sina kesho kutwaliwa,
Sina kazi sina shina, wala tawi kuchipuwa,
Sina wanangu mi sina, la kwacha na kuraduwa,
Mrithi nini wanangu?

6. Sina utu sina haki, mila yangu 'meuliwa,
Nyumba yangu ili dhiki, na mbele imekaliwa,
N'nawana namiliki, hadi nitapofukiwa,
Mrithi nini wanangu?

7. Sina la kesho kwenu, wenyewe kuiongowa,
Muwane kwa nyingi mbinu, mwende pasi kupumuwa,
Leo siyo kesho yenu, kama mutajikakamuwa,
Mrithi nini wanangu?

Maswali

- (a) Andika kichwa kingine kifaacho kwa shairi hili (alama 1)
- (b) Shairi hili laweza kuwekwa katika bahari mbili tofauti. Zitaje na ueleze sababu ya kuliweka katika bahari hizo. (alama 4)
- (c) "Poleni wanangu sana, sina kwenu cha kutowa."
(i) Andika maneno haya kwa lugha nathari/ tutumbi/ lugha ya mjazo.(alama 1)
(ii) Utaje uhuru wa kishairi aliotumia mshairi katika kuyaandika maneno ya mshororo huo. (alama 2)
- (d) Taja tamathali ya usemi iliyotumika katika kibwagizo cha shairi hili. (alama 1)
- (e) Eleza dhamira (sababu kuu) ya mshairi kulitunga shairi lenyewe. (alama 2)
- (f) Eleza kwa ufupi maisha ya mshairi yalivyo. (alama 3)
- (g) Ni yapi matumaini ya mshairi kwa wanawe? (alama 2)
- (h) Eleza matumizi ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika shairi hili.(alama4)
(i) Mkata
(ii) Shakawa
(iii) Mana
(vi) N'tapofukiwa.
- (i) Onyesha jinsi uhuru (idhini) wa ushairi ulivyotumika katika shairi hili. (alama 4)
- .

Maswali ya Ziada:i) Taja mbinu zozote tatu za lugha alizotumia mshairi. (alama 3)

ii) Chambua umbo na muundo wa shairi hili. (alama 4).

7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

ILIMU

1. Ewe risala wa vina, upesi ngiya mjini,
Waleleo 'kiwaona, wazinduwe maaoni,
Kisha uwape bayani, ya faida muthamini,
Wajuwe ya kuwa fani, ni bahari 'so ufu.
2. Ilimu ni kitu chema, kuwa macho duniyani,
Hukuza wenyewe kusoma, popote ulimwenguni,
Msinayo huwa nyuma, hususa hizi zamani,
Tusomeni japo fani, ni bahari 'so ufu.
3. Ilimu ni taa mbake, yenye mng'aro wa shani,
Huongoza wanawake, na waume duniyani,
Msinayo naitake, ya dunia na ya dini,
Ilimu ulimwenguni, ni bahari 'so ufu.
4. Ilimu ndiyo mlango, wa mangi ulimwenguni,
Ina kikuu kiwango, cha shani iso kifani,
Msinayo huwa tongo, apapapsapo haoni,
Mkuza bongo ni fani, ni bahari 'so ufu.
5. Ilimu ni mali bora, yenye ifadi yakini,
Hukupanuwa fikira, na maarifa bongoni,
Kuikosa ni hasara, ubora tuitangeni
Tujuwe ya kuwa fani, ni bahari 'so ufu



6. Tamati hapa 'takoma, nduzangu kumbushaneni,
Na nyoyo tufanye hima, ya kwenda
madarasani, Tukadurusu uluma, za kutufaa
mbeleni, Maana cheo cha fani, ni bahari 'so
ufuo.

Maswali

- (a) Eleza arudhi za shairi hili. (alama 4)
- (b) Ni nini dhamira ya mwandishi wa shairi hili? (alama 2)
- (c) Taja hasara za kukosa elimu kwa mujibu wa shairi hili. (alama 3)
- (d) Taja aina za elimu zilizogusiwa katika shairi hili. (alama 2)
- (e) Mshairi ana maana gani anapoandika, "....bahari 'so ufuo." (alama 2)
- (f) Eleza matumizi ya tamathali zozote tatu za usemi katika shairi (alama 3)
- (g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi hili. (alama 4) (i)
Muthmini
- (ii) Mbake
(iii) Mketo
(iv) Uluma

8. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

PANDA

1. Panda, panda la mnazi, l'anzalo kupapatuwa,
Panda juu ya malezi, moyo wako wishe ngowa,
Panda mti wa mapanzi, uwepushie na juwa,
Panda ni wako uluwa, panda darajani, panda!

2. Panda juu ya farasi, kwa haiba na sitawa,
Panda kiwango mkwasi, uukimbie ukiwa,
Panda, situpe viasi, wndako ukikujuwa,
Panda ni wako uluwa, panda darajani, panda!

3. Panda ngano na mpunga, afudhali ya viliwa,
Panda wimbi na kimanga, vipawa vyta kupewa,
Panda, usitunde ch'anga, tauwa mbivu tauwa.
Panda ni wako uluwa, panda darajani, panda!

4. Panda mwema mshajari, wite t'anzu na mauwa,
Panda utunde johari, mwivi' asijezanguwa.
Panda juu ya mimbari, ulingane sawasawa,
Panda ni wako uluwa, panda darajani, panda!

Maswali

- (a) Taja na ueleze bahari za shairi hili. (alama 6)
- (b) Eleza maana mbalimbali za neno 'panda'kama zinavyojitokeza katika shairi.(Alama4)
- (c) Eleza matumizi ya ritifaa katika ubeti wa kwanza. (alama 2)
- (d) Eleza vina na mizani ya beti mbili za kwanza (alama 3)
- (e) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi: (alama 3)
(i) Daraja
(ii) Uluwa
(iii) Tauwa
- (f) Mtunzi ametumia tabdila na mazida katika kazi yake. Andika mfano kwa kila moja kama inavyojitokeza katika shairi. (alama 2)

9. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

NYAMA NJE NGOZI NDANI

1. Hicho ni kitu nasema, maarufu duniani,
Ni kikubwa chake kima, si kidogo wastani,
Tena ni kitu cha nyama, kina ladha mdomoni,
Nyama nje ngozi ndani, kitu gani wajuzi?

2. Mfano nawatajia, hasa kwa yake launi,
Rangi yake kahawia, inapendeza machoni,
Kwa tamu na rangi pia, kimefanana na ini,
Nyama nje ngozi ndani, ni kitu gani wajuzi?

3. Watu hukipenda sana, ni kitoweo nyumgni,
Si kirefu si kipana, si duara kama peni,
Na muda ukikiona, nyama nje ngozi ndani,
Nyama nje ngozi ndani, ni kitu gani wajuzi?

4. Hususa kwa kwetu huku, yaani bara na pwani,
Twakipenda kwa shauku, wala hapana kifani,

Chapatikana kwa kuku, ama ndege wa mwituni,
Nyama nje ngozi ndani, ni kitu gani wajuzi?

5. Na kwa hizi beti tano, ndipo pangu nasaini,
Yatosha huo kfano, ambao nimebaini,
Sasa yetu maagano, kunipa jibu yakini,
Nyama nje ngozi ndani, ni kitu gani wajuzi?

Maswali

- (a) Shairi hili ni la bahari gani? (alama 4)
- (c) 'Kitu' kinachozungumziwa' hutumiwaje? (alama 2)
- (d) Eleza dhamira ya shairi hili. (alama 4)
- (e) Andika ubeti wa nne kwa lugha ya nathari. (alama 4)
- (f) Toa maana ya msamati huu kama ulivytumiwa katika shairi . (alama 5)
- (i) Kima
 - (ii) Launi
 - (iii) Kahawia
 - (iv) Hususa
 - (v) Shauku

10. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

1. Ah! siambile ovyo, samba ah! kupuuzwa,
Ah! hii niambavyo, si kwamba nimependezwa,
Ah! moyo wamba hivyo, kwayo nilivyofanyizwa,
Ah! namba nionavyo, vipasavyo kuelezwu
2. Ah! mimi nilivyo, mawazo yametatzwa,
Ah! tata za magovyo, fikira zimeshangazwa,
Ah! na viwe viwa'vyo, sioni pa kutulizwa,
Ah! namba nionavyo, vipasavyo kueleza.
3. Ah! silili yavyo, kwa kutaka kunyamzwa,
Ah! sipendewi navyo, sipendewi kubewa,
Ah! ni hivi ambavyo, mkata heshi kutezwa?
Ah! namba nionavyo, vipasavyo kuelezwu.



4. Ah! kukicha ya vivyo, na uchao yajalizwa,
Ah! havishi vishavyo, na matayo kuambizwa,
Ah! sivyo hivi sivyo, vyakanywa na kukatazwa,
Ah! namba nionavyo, vipasavyo kuelezwা
 5. Ah! lau hata ndivyo, basi hata kulekezwa
Ah! wayaenda kwavyo, kwamba ndiko kutukuzwa,
Ah! tenda utendavyo, ni kuwa watendekezwa,
Ah! namba nionavyo, vipasavyo kuelezwা.
 6. Ah! ni vile wambavyo, togo upate tangazwa,
Ah! kila upendavyo, mwisho 'we utatukiziwa,
Ah! pendo liangazavyo, vipasavyo kuelezwা.
Ah! namba nionavyo, vipasavyo kwelezwa.
 7. Ah! kila lenye govyo, halikawili kuvizwa,
Ah! nalende lendavyo, ukomo litagotezwa,
Ah! ni viyi kulivyo, kukudumu kutulizwa?
Ah! namba nionavyo, vipasavyo kuelezwা.
 8. Ah! dunia ni kuyovskyo, kizamacho chaibuzwa,
Ah! ni mangapi ja 'vyo, hayako metokomezwa,
Ah! jaa lijaavyo, mwishilio lapunguzwa,
Ah! namba nionavyo, vipasavyo kuelezwা.
 9. Ah! kaa ukaavyo, hatimayo yasogezwa,
Ah! na uwe uwavyo, atendae hulipizwa,
Ah! hakuna liliyvo, gumu lisilosogezwa,
Ah! namba nionavyo, vipasavyo kuelezwা.
- Maswali na majibu**
- (a) Taja na ueleze tamathali zozote tatu zilizotumiwa na mshairi. (alama 6)
- (b) Mshairi analalamikia nini? (alama 3)
- (c) Huku ukitoa mfano kutoka shairi hili, eleza matumizi yoyote mawili ya uhuru wa kishairi. (alama 2)
- (d) Kwa nini anayezungumziwa anayatenda ayatendayo? (alama 3)
- (e) Eleza mana ya kibwagizo cha shairi hili. (alama 2)
- (f) Eleza msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika shairi. (alama 4)

- (i) Kutezwa
- (ii) Namba
- (iii) Watendekezwa
- (iv) Togo

11. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

1. Tusitake kusimaima, bila kwanza kutamba,
Au dede kuwa hima, kabula hatujakaa,
Tutakapo kuchutama, kuinama inafaa, Tujihimu
kujinyima makubwa kutoyavaa.

2. Tusitake kuendea, guu lisipokomaa,
Tujizonge na mikanda, inapochagiza njaa,
Na mazuri tukipenda, ni lazima kuyaanda,
Tujiase kujipinda, kujiepusha na balaa.

3. Tusitake uvulana, au sifa kuzagaa,
Tushikiye nyonga sana, tunuiyapo kupaa,
Kama uwezo hapana, tutolee dagaa, Tujiase hicho
kina, maji yajapokujaa

4. Tusitake vya wenzetu, walochuma kwa hadaa,
Wanaofyatua vitu, na kisha vikasambaa,
Uwezo hatuna katu, umasikini fazaa, Tujihimu kula
vyetu, siendekeze tamaa.

5. Mtaka kuiga watu, kufata kubwa rubaa,
Vyao vijile kwetu, vifaa vingi vifaa, Tunamezwa na
machatu, tusibakishwe dhiraa, Tujihimu kilo chetu, hata
kama twapagaa.

Maswali na majibu

(a) Toa kichwa mwafaka cha shairi hili (alama 1)

(b) Eleza vina na mizani vya ubeti wa kwanza na wa mwisho (alama 4)

(c) Shairi hili lina bahari tofauti. Zitaje na uthibitishe. (alama 4)

(d) Eleza dhamira ya mshairi katika shairi hili. (alama 2)

(e) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha nathari. (alama 4)

Tusitamani kusimama kabla ya kutambaa au kusimama kabla hatujakaa. Tunapotaka kuchutama lazima tuiname. Tujifunze kujinyima yale ambayo hatuyawezi

(f) Taja uhuru mmoja wa mshairi kama unavyojitokeza katika ubeti wa nne. (alama 2)

(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa. (alama 3)

(i) Dede

(ii) Tujizonge

(iii) Kuiga .

12. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

MALI

1. Kupenda mno ukwasi, naona nitapotea, Mali ina wasiwasi, na laweza kupotea, Mali huzua *maasi*, mtu yakampotoa.

2. Mali ni njema hidaya, hili kweli nalijua, Sura yangu iwe mbaya, watu wataisifia, Lakini naona haya, sifa hii kupokea.

3. Mali ni nzuri hidaya, tena ninkariria, Lakini ina *hekaya*, ngumu kuizingatia, Hususa huwa *kayaya*, dunia kuizamia.

4. Mali pale niko nayo, wengi walininamia, Bali nikitokwa nayo, rafiki wanikimbia, Na nipigapo miayo, pemberi wanizomea.

5. Mwenye mali huzuzuka, kheri akaziambaa, Na heshi kubabaika, kushukushuku jamaa, Na huko kafilisika, akuhofu kila saa.

6. Umesikia karuni, dongo likamfukia, Mali ilimfitini, dongo likamfukia, Ni khatari yumkini, kwa sababu ya rupia.

7. Maadui wa mkwasi, ni wengi kupindukia, Rafikize si halisi, *ghalibu* humdowea, Wamchomoe *fulusi*, kisha wamtete pia.

8. Kheri nikidhiwe haja, shida zikinifikia, Nile kadiri ya
haja, na nione njaa pia,
Na niipate faraja, dhiki zikinitokea.

9. Ewe Mola wangu Bwana, Jalla wa ala Jalia Ufukara
Maulana, nakuomba nepushia, Nipe riziki mwanana, haja
kunitoshelea.

10. Ukinipa utajiri, nipe na elimu pia,
Mali zangu niajiri, ziwafalie insia,
Nishukuru Qahari, vile kunifadhilia.

Maswali

(a) Eleza sifa za shairi la aina hii. (alama 3)

(b) Mwandishi ameeleza madhara na manufaa ya kuwa na mali. Taja madhara sita na
manufaa matatu. (alama 9)

(c) Mshairi anaomba nini kutoka kwa Mola katika bet tatu za mwisho? (alama 3)

(d) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivytumika katika shairi hili. (alama 5)
(i) Maasi

(ii) Hekaya

(iii) Kayaya

(iv) Ghalibu

(v) Fulusi

13. Soma shairi lifuatato kisha ujibu maswali.

PENDA CHAKO

1. Kukipenda kitu chako, huo ndio uzalendo,
Mtu anapenda chake, japo hakina thamani.
Hatamani cha mwenzake, na kukitia rohoni,
Chake ni furaha yake, huo ndio uzalendo.

2. Kuipenda nchi yako, huo ndio uzalendo,
Kuwa tayari daima, taifa utumikia,
Uzukapo uhasama, haraka kupigania,
Adui kuwasakama, mbali kuwatupilia.

3. Kuwapenda watu wako, huo ndio uzalendo,
Uzalendo ndio ngao, ni silaha kamilifu,

Tuwe nao moyo huo, tusiwe nyoyo dhaifu,
Wale wakilinda kwao, nasi tuwe timilifu.

4. Kukipenda kazi yako, huo ndio uzalendo,
Kazi tusitegee, ni uhai na afia,
Mazalendo jitoee, hasa shamba kulimia,
Fanya kazi harambee, kwa uchumi kuinua.

5. Kuipenda lugha yako, huko ndio uzalendo,
Tupendane kwelikweli, hakuna kubaguana,
Ukabila tusijali, sisi sote twafanana.
Tutumie Kiswahili, rahisi kuelewana.

6. Kupenda taifa lako, huo ndio uzalendo,
Uzalendo ni upole, mapenzi kwa nchi yako,
Si ubishi wa kelele, vituko na maudhiko,
Nchi haisongi mbele, uzalendo sipokuwepo.

Maswali

- (a) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha ya nathari. (alama 4)
- (b) Shairi hili lina umuhimu gani kwa taifa la Kenya? (alama 4)
- (c) Ni tamathali gani ya usemi iliyotumika katika mshororo:
(i) "Uzalendo ndio ngao, ni silaha kamilifu."? (alama 1)
- (ii) Eleza sababu za jibu lako kwa swali la (c) (i) (alama 3)
- .
- (d) Eleza sifa za kiarudhi kama zilivyotumika katika ubeti wa sita. (alama 4)
- (e) Ni nini maana ya mshororo "Wale wakilinda kwao, nasi tuwe timilifu"? (ub. 3) (alama 1)
- (f) (i) Taja mifano yoyote miwili ya maneno yaliyotumiwa kwa maksudi ya ulinganifu wa vina katika shari hili. (alama 2)
(ii) Eleza maana ya neno 'kuwasakama' kama iliyotumiwa katika shairi hili.
(alama 1)



14. Soma mashairi yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.

POLE RAFIKI

1. Nakupa pole sahiba,
Ulokusibu msiba,
Kifo mkeo kamwiba,
Kakuacha ukilia.
2. Mauti hana imani,
Na hakwambii ni lini,
Ukajuwa siku gani,
Ghafula hukuvamia.
nyumbani kwako,
jiko, Apate mshufaia.
Kakwacha na sikitiko,
Na mengi kufikiria.
4. Sieke moyo machungu,
Sikia rafiki yangu,
Bali mshukuru Mungu,
Hicho ndicho kidunia.
mulipendana,
Hata sisi tuliona,
Lakini sasa hakuna,
Mwenye kukurudisha,
kupenda,
Kukakuranya kukonda,
- Kiwa ni la moyo donda,
Mwana alilokwachia.
7. Mkeo hakupotea,
Hilino la kuelea
Bali ye ye karegea,
Kwa Mola wake Jalia
8. Badala ya kukufuru,
Yakupasa ushukuru 3. Kangia
Umuombee Ghafuru, Kamtwaa mwenye
9. Tumuombee Rahamani,
Ampe yake imani,
Amjalie peponi,
Nyumba ya wema jamia.
10. Iliyobakia na wewe,
Ijapo si mfanowe, 5. Najuwa
Nyumbani tasaidia.
11. Sikiza sakubimbi,
Na ya kwao tumbi tumbi,
Bilashi tapata dhambi, 6. Usikuache
Kwa mawi kuyawazia.

MWANA YATIMA

1. Likuwa katika dunia,
Dunia alonotoa.
2. Likiwa katika dunia,
Wa ziwa lake kubugia.
3. Lilikuwa katika dunia,
Wa njaa kuniondolea.
4. Likuwa katika dunia,
Kilio changu alojua.
5. Lilikuwa katika dunia,
kunijaza.
6. Likuwa katika dunia,
Kionewa kunitetea.
7. Sinaye katika dunia,
kunivua.
8. Sinaye katika dunia,
Bahari janga kunipoa.
9. Sinaye katika dunia,
Kunipa wakeo wasia.
10. Sinaye katika dunia,
Kwenye ndoa kunandalia.
11. Sinaye katika dunia,
Kuniombea jema dua.
12. Hayupo katika dunia,
Shiria tuli limetulia.
13. Hayupo katika dunia, Wa faraja
Uyatima kanimwaia.
14. Kaachwa katika dunia,
Kabaki tu na ning'inia
15. Kaachwa katika dunia, Waingiyani
Hivyo kitawi kasinyea.
16. Kaachwa katika dunia,
Miye kitawi tashikani?

Maswali

(a)(i) Linganisha mashairi haya kwa upande wa umbo. (alama 3)

(b) Taja wahusika wa mashairi haya. (alama 2)

(c) Mshairi wa Mwana Yatima amefiwa na mzazi. Ni mzazi yupi? Eleza. (alama 2)

(d) Taja na kufafanua mbinu zozote tatu za lugha zilizotumiwa katika mashairi yote mawili. (alama 6)

(e) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika mashairi. (alama 4)

(i) Ghufuru

(ii) Tumbwi tumbwi

(iii) Ziwa

(iv) Tasinyaa

15. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

KIBURI

1. Kiumbe utahadhari, ushike ninalonena,

Uwache zako ghururi, tena zingatia sana,

Kuwa si chema kiburi, na masilahi hakina, Ni bora

kuambizana, mja kiburi si chema.

2. Nakupa langu shauri, ambalo ni la maana,

Kaa na wendo vizuri, pasipo kuchukiana,

Tena uliwache kori, tabia ya kujivuna,

Ni bora kuambizana, Mja kiburi si chema.

3. Aringaye afikiri, ya kuwa salama hana,

Atamrudi kahari, duniani tukiona,

Na kiama kikijiri, dhiki yamngoja tena,

Ni bora kuambizana, mja kiburi si chema.

4. Hili ujue dhahiri, usidanganyike bwana,

Waja wote ni kadiri, alowaumba Rabana,

Za nini zako fahari, kwa kutaka kuza jina,

Ni bora kuambizana, mja kiburi si chema.

5. Usijione tajiri, kwa yako hiyo hazina,

Ama kuwa ni waziri, waringa ukitukana,

La mwanzo lina ahiri, ewe mja zindukana,

Ni bora kuambizana, mja kiburi si chema.

6. Wangapi walokithiri, wale wakitajikana,
Walokuwa na amri, wenye afia na zana,
Zimekoma takaburi, arighi imewabana,
Ni bora kuambizana, aridhi imewabana.

7. Kaditama wacha ari, ambayo ni ya laana,
Uwache zako jeuri, na kiburi epukana, Uwe ni mtu mzuri,
kwa wazee na vijana, Ni bora kuambizana, mja kiburi si
chema.

Maswali

- (a) Mwandishi anatoa sababu gani za kueleza kuwa mtu aepuke na kiburi (alama 3)
- (b) Eleza maana inayojitokeza katika maneno yafuatayo: (alama 4)
 - (i) "La mwanzo lina ahiri, ewe mja zindukana."
 - (ii) "Kaa na wendo vizuri, pasiwe kuchukiana."
- (c) Mwandishi anatoa ushauri gani kwa mtu mwenye kiburi? (alama 2)
- (d) Kwa nini msanii ametumia neno *afia* badala ya afya katika ubeti wa sita? (alama 1)
- (e) Andika ubeti wa sita kwa lugha ya nathari. (alama 4)
- (f) Eleza kanuni zilizotumiwa kusarifu ubeti wa kwanza (alama 4)
- (g) Andika maaana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika shairi. (alama 2)
 - (i) Ghururi
 - (ii) Ari

16. Soma mashairi yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.

SHAIRI 'A'

1. Upendacho hupendeza, japo kibaya machoni,
Hakini kukichukiza, pendo liwapo moyoni,
Pofu huitia kengeza, watu wakaona shani,
Kipendacho moyo dawa, pofu huita kengeza.
2. Waja kukuliza, macho yake hayaoni?
'Mtu huyu ameoza, 'yangu yawahusiani?' Budi utawajibiza,
'yangu yawahusiani?' Kipendacho moyo dawa, pofu huita
kengeza.
3. Sababu zao bughudha, hutaki nao utani,
Kujua hapana radhi, ya kila rohoni,

Ni hali gani orodha, isiyo na walakini,
Kipendacho moyo dawa, pofu huita kengeza.

4. Kingawaje maridhawa, pofu huita kengeza.
Ni hali yenye usawa, maisha kisitawini,
Moyo unachopotowa, tajiri maskini,
Kipendacho moyo dawa, pofu huita kengeza.

SHAIRI 'B'

1. Lau kwamba waelewa, lililo mwangu moyoni
Katu hungalitobowa, kueleza hadharani,
Apendaye hana dawa, mwenye kupenda haoni,
2. Haoni na hasikii, hafui wala hashoni,
Hendi wala hakimbii, haogi na hatamani,
Kuzuia kii kii, wangasema majirani.
3. Majirani wanganena, humtia midomoni
Na hata habari hana, msemaji asilani,
Yuko tuli amebegana, awatazama machoni.
4. Machoni awatazama, kuwajibu katiwaani,
Ni bure mngesema, mwajiudhi ikhiwani,
Basi hapa kaditama, ndugu zangu kwaherini.

Maswali

- (a) Tofautisha na ulinganishe mashairi haya kwa upande wa:
(i) Maudhui
(ii) Muundo/ umbo. (alama 10)
- (b) Andika methali mbili zinazorejelewa katika mashairi haya. (alama 2)
- (c) Andika ubeti wa nne katika shairi la 'B' kinathari. (alama 3)
- (d) Taja uhuru wa mwandishi alioutumia kuandika neno 'hungalitobowa' (ub.1 'B') na sababu ya kuliandika hivyo. (alama 2)
- (e) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika shairi hili. (alama 3)

- (i) Sababu zao bughudha
- (ii) Maridhawa
- (iii) Humtia midomoni

17. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

1. Lipi la kutenda, kwa walimwengu, liwe jema? Liwe ni
kupenda, bila uchungu, na lawama Niwe kama punda,
pasipo fungu, wala kima.
2. Lipi lisilo inda, kwa walimwengu, na lazima? Liwe la kuonda,
kukupa Mungu, lisokwama, Laiti si winda, enyi nduzangu,
lau kama.
3. Kipi cha kupanda, kwa walimwengu, cha salama? Kiwe
kama tunda, au furungu, la mtama, Hata zao nyonda,
ziunge zangu, na kuvama.
4. Ni wapi pa kwenda, kwa walimwengu, pa huruma, Niwe ni
kupanda, daraja yangu, pasi vuma, Pasiwe na chonda, ajae
kwangu, kwa dawama.
5. Upi pa kudanda, kwa walimwengu, pasi kwima?
Na kuvuta nyanda, ziso wenzangu, 'pite wima,
Kwa kurandaranda, niwape dungu, wawe nyuma
6. Lipa la kushinda, kwa walimwengu, kiwe chuma? Bila ya
kuponda, kwa kilimwengu, na hikima, Na lau wadunda,
weshe mizungu, ni kizima.
7. Kipi kisovunda, kwa walimwengu, cha daima? Pasi na
kukonda, kwa malimwengu, yaso wema, Angawa ni
nunda, huja kiwingu, cha makama.

Maswali

- (a) Taja hoja zozote nne ambazo mwandishi anazishughulikia katika shairi. (alama 4)
- (b) Eleza sifa za kiarudhi katika ubeti wa pili. (alama 6)
- (c) Andika ubeti wa nne kwa lugha ya nathari. (alama 4)
- (d) Kwa nini mshairi anatumia maneno 'nduzangu' (ub. 2) na 'yaso' (ub. 7) ? (alama 2)
- (e) Ni kwa nini mshairi anauliza swali katika mwanzo wa kila ubeti? (alama 1)
- (f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika shairi: (alama 3)
- (i) Inda
- (ii) Nyonda
- (iii) Mizungu

18. Soma shairi lifuatalo yanayofuata kisha ujibu maswali.

ULIMI

1. Ulimi bayana, nyoka mo pangoni, limtoa,
Ulimi wangwana, hapo barazani, kuongea,
Ulimi lishana, kiwa furahani, sherekeea,
Ulimi kaziye.
2. Ulimi tapika, yo majungu sana, kipakua,
Ulimi sifika, kubuni hufana, kisikia,
Ulimi hutaka, na chumvi zadina, chuku pia,
Ulimi kaziye.
3. Ulimi salata, kwake mwenye nao, huchongea
Ulimi, huleta, kwa wasengenyaao, singizia,
Ulimi matata, na wagombanao, lipizia,
Ulimi kaziye.
4. Ndimi kiwa mbili, mithili kinyonga, geukia,
Ndimi ziso kweli, jama za kukenga, huhadaa,
Ndimi hazibali, mara huvinga, ni balaa,
Ulimi kaziye.
5. Ulimi twambiwa, kizungumkuti kufanyia,
Ulimi tambuwa, tazungukwa mti, kizingia,
Ulimi tambuwa,tazungukwa mti, kizingia,
Ulimi ungwana, kinywani mo kati, tamkia
Ulimi kaziye.

Maswali

- (a) Eleza kazi ya ulimi kwa mujibu wa shairi hili. (alama 4)
- (b) Taja tamathali za usemi zilizotumia katika mishororo ifuatayo.

(c) Eleza arudhi alizotumia mshairi katika ubeti wa tatu. (alama 6)

(d) Shairi hili ni la bahari ya kikwamba. Thibitisha. (alama 2)

(e) Andika ubeti wa nne kwa lugha ya nathari. (alama 4)

(f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivytumiwa katika shairi hili. (alama 2)

(i) Wangwana

(ii) Huchongea.

19. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

UKUBWA JAA

1

Dunia yetu dunia, watu wanakufitini,
Dunia huna udhia, watu wanakulaani,
Dunia huna hatia, wabebeshwa kila zani,
Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

2

Dunia umenyamaza, umetua kwa makini,
Dunia vitu 'mejaza, watu wanataka nini?
Dunia wanakucheza, insani maliuni,
Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

3

Dunia mtu akose, hukutia mdomoni,
Dunia hebu waase, hao watu mafatan,
Dunia chuki mpuse, muipate afueni,
Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

4

Dunia una lawama, za uongo si yakini,
Dunia wanokusema, ni manjunju si razini,
Dunia huna hasama, waja ndio kisirani,
Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

5

Dunia kuharibika, hayo amezusha nani?
Dunia watu humaka, hao wanaokuhini,
Dunia umejazika, kila tunu ya thamani,

Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

6

Dunia unatulisha, bwerere bila undani,
Dunia unatukosha, maji tele baharini,
Dunia unaotesha, mimea tosha shambani,
Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

7

Dunia hujageuka, tangu umbwe na manani,
Dunia watu ndo nyoka, mahaini na wahuni,
Dunia una Baraka, mwenye pupa hazioni,
Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

Maswali

- (a) "Mbaazi ukikosa maua husingizia mvua au jua." Thibitisha ukweli wa methali hii kwa kuzingatia yale yanayosemwa katika shairi hili huku ukihusisha maana ya kichwa cha shairi. (alama 6)
- (b) Kwa nini watu hutupia dunia lawama zote? (alama 2)
- (c) Shairi hili linadhahirisha hulka gani ya mwanadamu? (alama 2)
- (d) Eleza arudhi zilizofuatwa katika kutunga shairi hili kwa kuzingatia vina, mizani, uhuru wa ushairi, bahari. (alama 5)
- (e) Eleza maana ya msamati uliopigiwa msitari kama ulivyotumika katika shairi. (alama 5)
- (i) Zani
(ii) Mafatani
(iii) Manjunju
(iv) Bwerere
(v) Insani

20. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

JUZI NA JANA SI LEO

1. Ewe mwanati zinduka, usingizi uleleo,
Upate kunipulia, haya yangu kwa *kituo*,
Na iwapo kutoshika, basi tena ni weleo,
Juzi na jana si leo, zigeushiye zamani.

2. Zinduka utafakuri, uwate ushishiyeo,
Uvivu *usikughuri*, Jitenge usende nao,
Ukiandama *usiri*, utapitwa na wendao,
Juzi na jana si leo, zigeushiye zamani.

3. Hela onyo moyo wako, ukiri la malekoo,
Utizame na wenzako, wendavyo maendeleo,
Na wewe upange yako, uwe mbele kama wao,
Juzi na jana si leo, zigeushiye zamani.
4. Iwapo hutojipinda, kutaka maendeleo,
Wenye yao 'takushinda, wakuwate nyuma yao,
Ubaki kuuma *vyanda*, kama wale wajutao,
Juzi na jana si leo, zigeushiye zamani.
5. Ambaye hashughuliki, kuwa mema maendeleo,
Na akawa ashiriki, uvivu alionao,
Basi huwa heshi dhiki, wala hawi na kituo
Juzi na jana si leo, zigeushiye zamani.
6. Dunia yetu hakika, kwa wakati taonao,
Aso kamba ya kushika, katika maendeleo,
Jina lakwe huanguka, kikamshuka na cheo,
Juzi na jana si leo, zigeushiye zamani.
7. 'Takupa mfano shika, ufikiri kwa kituo,
Yeyote mwenye kutaka, kulima awe endao,
Aketipo huenuka, kisha 'kenda muda huo,
Juzi na jana si leo, zigeushiye zamani.
8. Kadiratami shairi, sineni mengi kwa leo,
Jina langu mashuhuri, mtungaji kwa *kituo*,
Ni Ahmadi Nasiri, Juma Bhalo nitajwao,
Juzi na jana si leo, wanati zinduwanani.

Maswali

- (a) Shairi hili ni la bahari gani? (alama 2)
- (b) Eleza maudhui ya shairi hili (alama 2)
- (c) Huku ukitoa mifano, eleza matumizi ya:

(i) Mazida (alama 2)

(ii) Inkisari. (alama 2)

(d) Ni methali gani inayorejelewa katika ukwapi wa kibwagizo cha shairi hili? (alama 2)

(e) Eleza ujumbe unaojitokeza katika ubeti wa saba. (alama 2)

(f) Uandike ubeti wa nne kwa lugha ya nathari. (alama 4)

(g) Eleza maana ya msamati ufuatao kama ulivytumiwa katika shairi. (alama 4)

(i) Usikughuri

(ii) Usiri

(iii) Vyanda

(iv) Kituo

21. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

1

Uache kuhadaika, kwa haraka umaizi,
Soma na kuelimia, ili upate ujuzi,
Upate kunufaika, uepuke na upuzi.

2

Uepuke ya upuzi, uwe mtu wa dunia
Elimu kitu *azizi*, asiyejua ni nani?
Kuanzia ya malezi, hadi elimu chuoni

3

Hadi elimu chuoni, ulifinze ya maana
Uepuke ujingani, ujahili sio ungwana,
Na elimu nyumbani, jifunze toka ujana.

4

Jifunze toka ujana, kutokana na wazazi,
Ujue vyema kunena, tena uwe msikizi,
Na adabu shikamana, uwache ya ubazazi.

5

Uwache ya ubazazi, upate kutimilia na kila,
Na kila lenye *ajizi*, uvivu kuuchukia,
Pia pambo la kivazi, usafi kuutumia

6

Usafi kuutumia, wa nguo hadi wa mwili,
Ushike na ya sheria, ibada yake *Jalali*,
Na elimu ya dunia, ujifunzd kila hali,

7

Ujifunze *kulihali*, hapa ndipo kituoni,
Hakuna kitu cha mali, kama elimu jamani,

Ya dini ya awali, ya pili ni ya dunia.

Maswali

- (a) Andika anwani mwafaka ya shairi hili (alama 2)
- (b) Onyesha jinsi mtunzi wa shairi hili alivyofaulu katika kuzingatia arudhi za utunzi wake. (alama 6)
- (d) Andika ubeti wa nne katika lugha nathari. (alama 4)
- (e) Eleza maaana ya maneno yafuatayo kama yaliviyotumiwa katika shairi. (alama 5)
- (i) Kuhadaika
- (ii) Azizi
- (iii) Jalali
- (iv) Kulihali
- (v) Ajizi

22. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

MTEGO

1. Kalamu tungali nazo, usambe zimekatika,
Tuyaonapo mauzo, kujibu hatuna shaka,
Matumbo na mageuzo, Si yenye kutuzunguka,
Mtego ulomshika, kesho utashikwa wewe.

2. Kesho utashikwa wewe, mwenzio ulomshika,
Ghafula usijuwe, mtego umefyatuka,
Na jina bayu upewe, usitake ukitaka,
Mtego ulomshika, kesho utahikwa wewe,

3. Tumeudhika wenzio, kwa yale ulotamka,
Washangilia kilio, nduguyo kilomfika,
Wampigia havio, hadharani wameheka,
Mtego ulomshika, kesho utashikwa wewe,

4. Mila na sheria zetu, zakataza kujicheka,
Na wewe umethubutu, makala kuyaandika,
Jikumbuko mwanakwetu, au umeghafilika,
Mtego ulomshika, kesho utashikwa wewe.

5. Sisi twaona aibu, na wewe washereheka,
Nduguyo umemsibu, kwa jambo liso hakika,
Na hii ndiyo sababu, kusahau ulotoka,
Mtego ulomshika, kesho utashikwa wewe.

6. Kaditamati furaha, isije ikapunguka,
Ikasababisha siha, ulonayo kuyeyuka,
Ufanyiwe na mzaha, wakati waaiika,
Mtego ulomshika, kesho utashikwa wewe.

Maswali

- (a) Kwa maneno yako mwenyewe, fafanua maana ya kibwagizo cha shairi hili, "Mtego ulomshika, kesho utakushika wewe." (alama 2)

- (b) Eleza vina vya ubeti wa kwanza wa shairi hili (alama 2)

- (c) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari. (alama 4)
- (d) Thibitisha kuwa shairi hili linawezekutumiwa kama onyo na ushauri. (alama 4)
- (e) Kuna baadhi ya maneno yaliviyotumiwa na msanii kwa njia ya mkato. Taja maneno na ueleze kwa nini yametumiwa hivyo (alama 4) matatu

- (f) Eleza maana ya maneno haya kama yaliviyotumiwa (alama 4)
 - (i) Umefyatuka
 - (ii) Umeghafilika
 - (iii) Washereheka
 - (iv) Kaditamati

23. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

AJALI BARABARANI

1. Ajali si jambo bora, kutukia kwa yeote,
Huathiri kila mara, jamii na watu wote,
Hebu wacha masihara, sijesakamwa na mate,
Dereva kuwa makini, mbona watuhatarisha.

2. Ajali nyingi hujini, kwa mso mwangalifu,
Mtu hataki kukiri, ulevi naye ni kufu,
Yualipeleka gari, na mawazo yako dufu,
Dereva kuwa makini, mbona watuhatarisha?

3. Umepata dereva, gari kupeleka kasi,
'Ngadhani mamba haiva, ahera, pamoja nasi,
Kaonyesha udereva makini, kuvuma kwa pepe kusi,
Dereva kuwa makini, mbona watuhatarisha?
 4. Sishutumu dereva tu, bali na wapita njia,
Akili kuwa ja butu, 'toheshimu barabara,
Yu mbioni kutukutu, na fikiraze kalala,
Dereva kuwa makini, mbona watuhatarisha?
 5. Basi sikuyo katimu, hiyo ya barabarani,
Hujui na wapi mumu, wala yalijini kwani,
Viungovsky kutodumu, vilivyokote mwilini
Dereva kuwa makini, mbona watuhatarisha?
 6. Watoto wao wabaki, bila mzazi yejote,
Yatima kindakindaki, na pia wajane wote,
Maisha hayanunuliki, kwa soko lolote kote.
Dereva kuwa makini, mbona watuhatarisha?
 7. Nami ustadhii bara, sinalo la kufanyani,
Kupoteza ua bora, la waridi ajalini,
Kutafuta na kuvara, sijui tapata lini,
Dereva kuwa makini, mbona watuhatarisha?
 8. Sote twajua kwa kweli, ajali haikingiki,
Mbona sifiki mbali, tuwe hakika kikiki,
Tusija tukakubali, jiletea taharuki,
Dereva kuwa makini, mbona watuhatarisha?
 9. Quaditamati khabari, nabaki humu kimyani,
Ukiitaka habari, Isome humu betini,
Sitaki kutaashiri, Qudusi kayaffuani,
Dereva kuwa makini, mbona watuhatarisha?
- Maswali**
- (a) Taja visababishi vinne vya ajali barabarani kulingana na shairi hili (alama 4)
- (b) Katika shairi hili kuna maneno ambayo hayajaandikwa kisarufi. Taja mifano minne.
(alama 4)
- (c) Chambua ubeti wa sita ukizingatia bahari, mizani, vina na mishororo na vipande.

(d) Andika ubeti wa tano kwa lugha ya nathari. (alama 4)

(e) Kwa nini maneno haya yamefupishwa? (alama 1)

(i) Sikuyo

(ii) Viungovsky

(f) Taja jina la Mungu lililotajwa katika shairi hili. (alama 1)

(g) Taja athari mbili zinazosababishwa na madereva kukosa makini. (alama 2) ☺ Kifo.

24. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

1. Ameumbwa mwanadamu, kwa lililo zuri umbo,

Bali si wote fahamu, waliyo na sawa mambo,

Wako waliyo timamu, na wengineyo wa kombo,

Na mtu kuwa na tumbo, si kwamba mekamilika.

2. Kuna walo mafidhuli, lugha yao ni matango,

Na kuna wenye kauli, zisizokuwa na ushingo,

Kuna kwake kwa wavuli, vipofu na wenye tongo,

Na mtu kuwa na shingo, si kwamba 'mekamilika.

3. Kuna waho na fikira, na wenye vibovu vitwa,

Kuna walo na subira, husubiri kucha kutwa,

Wengine tabiya bora, hino hawanayo katwa

Na mtu kuwa na kitwa, si kwamba mekamilika.

4. Kukamilika kwa mja, ni mbali na kwa Moliwa,

Kwa mja nitakutaja, ili upate kwelewa,

Ni kufikiya daraja, kile alichoumbiwa,

Hapo ndipo huambiwa, mja amekamilika.

5. Aiyelewe duniya, kwa marefu na mapana,

Azipite zile ndiya, za miba mitungu sana,

Avuke bahari piya, zilo na virefu vina,

Hiyo ni vyangu maana, ya mja kukamilika,

6. Akishafikwa na hayo, si kwamba ndiyo akhiri,
Lazima awe na moyo, wa kuweza kusubiri,
Kuyasubiri ambayo, yote yatayomjiri,
Kama huyo 'tamkiri, ni mja mekamilika.

Maswali

- (a) Kwa kuzingatia shairi hili, fafanua mambo muhimu yanayomfanya mtu kuwa na utu.
(alama 5)
- (b) Kuna uhusiano gani kati ya 'vibovu vitwa,' tabiya bora,' na mtu kuwa na kitwa' katika ubeti
wa tatu? (alama 4)
- (c) Msanii anakiri nini kuhusu mja? (alama 4)
- (d) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika shairi. (alama 3)
(i) Wavuli
(ii) Katwa
(iii) Akhiri
- (e) Andika ubeti wa 5 kwa lugha ya nathari. (alama 4)

25. Soma mashairi haya kisha ujibu maswali yanayofuata.

SHAIRI 'A'

1

Tajiri hajali duni, mnyonge mtu fakiri,
Duni wa hali ya chini, shaibu ama saghiri,
Humuita nusu nyani, na kuonyesha kiburi,
Utajiri ni Khamuri, baadhi yao hulewa.

2

Baadhi yao hulewa, hulewa kuwa chakari,
Hawajali wakiwa, hutoa zao jeuri,
Huona wanao mbawa, za kuruka kwa fahari,
Utajiri ni Khamuri, baadhi yao hulewa.

3

Wengine ni wafadhili, matajiri wenye kheri,
Maskini huwajali, na kumwogopa Khahari,
Wengine ni mafidhuli, hupati heri ni shari,
Utajiri ni Khamuri, baadhi yao hulewa.

4

Mali ikiwaishia, dhahabu na majohari,
Usikini hurudia, iwatokapo khamuri,

Hubaki kulialia, awachapapo kabiri,
Utajiri ni khamuri, baadhi yao hulewa.

SHAIRI 'B'

1. Akiwa na nguvu mtu, kwa mali ana dalili,
Atajipatia vitu, kimjalia Jalali,
Mwisho atapata utu, ufuke kuubadili,
Nguvu ya mtu ni mali, ni mali nguvu ya mtu.
2. Kwa kesho na keshokutwa, tabadili yake hali,
Alikuwa akisutwa, mshenzi aso akili,
Ni jamili ataitwa, na watu watamjali,
Nguvu ya mtu ni mali, ni mali nguvu ya mtu.
3. Ni mali ya mtu nguvu, mtu wa Rasilmali,
Ijapo si mshupavu, nguvu hanazo za mwilini,
Ingawa ni mlegevu, maliye itakabili,
Nguvu ya mtu ni mali, ni mali nguvu ya mtu.
4. Itakabili maliye, kumwondoa udhalili,
Japo hana nguvu yeye, nguvu zake ni kalili,
Kwa ile mali ambaye, tamfanya kukamili
Nguvu ya mtu ni mali, ni mali nguvu ya mtu

Maswali na majibu

- (a) Mashairi haya yanakinzana. Fafanua. (alama 8)
- (b) (i) Mungu amepewa majina mbalimbali katika mashairi. Yataje. (alama 3)
- (ii) Eleza umuhimu wa Mungu katika mashairi haya. (alama 2)
- (c) Fafanua misemo ifuatayo kama ilivyotumiwa katika mashairi haya. (alama 2)
- (d) Eleza sababu mbili zilizomfanya mshairi wa shairi la 'B' kutumia neno 'kukamili' katika ubeti wa 4 (alama 2)
- (e) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumia katika mashairi. (alama 3)
- (i) Shaibu
- (ii) Jamili
- iii) Kalili

26. Soma shairi hili kisha ujibu maswali.

SHAIRI 'A'

Nimeona, milima na mabonde, misitu na nyika, Nimeona, majani
na umande, uliotandazika, Nimeona, mkulima yuwenda shambani.

Nimeona, uwanda wa magugu, yalomkabili, Nimeona,
wajibu na vurugu, wiano mkali, Nimeona, mkulima
akiwa tayari.

Nimeona, kwa ari na juhudu, anatupa jembe, Nimeona,
kakaza ukaidi, kwa nguvu achimbe, Nimeona, mkulima
akiwa kazini.

Nimeona, kijua kinawaka, kama jehanamu, Nimeona, jembe
lainuka, linapohujumu, Nimeona, mkulima akiwa mbioni.

Nimeona, mvua yamiminika, nayo hatohis, Nimeona,
kwa nani anatimka, bila wasiwasi, Nimeona, mkulima
akiwa kazini.

Na sioni, jasho linapomwaika, yendapo mazao, Na sioni,
hadhiye kutukuka, ila kilio, Kwa nini? Nauliza mkulima:
Kwani?

SHAIRI 'B'

1. Wakati miaka inaibwa mmoja mmoja,
Kurudi nyuma, kusimama, kupunguza mwendo,
Siwezi, kama gurudumu nitajivingirisha,
Mtelemko mkali huu.
Lini na wapi mwisho sijui.
2. Mbele chui mweusi, nyuma mwanga
Nionako kwa huzuni vifurushi maelfu nya dhambi
Kisu, maisha kafiri haya
Kama kutazama nyuma au mbele
Ni kufa moyo.
3. Kama Simba-Mtu shauri nimeata
Nyuma sana nisijali, ya mbele sana niyakabili

Kwa ujasiri na uangalifu nitazunguka
Nikifuata-kamba kama ng'ombe aliyefungwa
Kila mpigo wa moyo wangu, Huu mpigo
muziki wa maisha.

Maswali

- (a) Onyesha tofauti zinazodhihirika katika mashairi haya kwa upande wa umbo/muundo.
(alama 5)
- (c) Ni taswira gani tunaweza kuipata tunapoyasoma mashairi haya?(alama 3)
- (b) Taja na ufanue tamathali tatu kutoka katika kila shairi. (alama 3)
- (d) Chambua maudhui ya mashairi 'A' na 'B' kwa kutoa mifano (alama 9)

27. Soma mashairi yafuatayo kisha ujibu maswali.

SHAIRI 'A'

Ufuke kwa mwanadamu, sumu ya kiwiliwili,
Kwa mwanadamu ni sumu, ufuke una ajali, Ufuke hufyonza
damu, mtu akawa dhalili, Ufuke kwa mwanadamu, sumu ya
kiwiliwili.

Mfuke haombi kitu, akapewa tasihili,
Japo jozi la viatu, aombe tafadhali,
Hunyimwa na kila mtu, sipate japo akali,

Ufuke kwa mwanadamu, sumu ya kiwiliwili.
Ufuke wawea uwa, ghafla bila muhali,
Watu mkashitukiwa, katoweka Bwana Ali, Na sanda ya
kuzikwa, kupata ikawa mbali, Ufuke kwa mwanadamu,
sumu ya kiwiliwili.

Ufuke una uchungu, lakini wa afadhali,
Midhali hauna fungu, umekaa pande mbili,
Si mweusi si Mzungu, sote tunajua hili,
Ufuke una kiburi, japo ye ye aliapa,
Ufuke kwa mwanadamu, sumu ya kiwiliwili.

SHAIRI 'B'

Siku yake atmake, ni lini atakulipa,
Hutamani atoroke, akospao pa kukopa, Angaahidi kulipa,
ufuke una kiburi.

Kukulipa alikiri, tena bila ya kukwepa, Utachoka
kusubiri, bado anatapatapa, Angaahidi kulipa, ufuwe
una kiburi.

Barazani utafika, kwa ahadi kutupa,
Utakata mashitaka, kukosa kwake kukupa,
Barazani taitika, hakuna cha kuogopa,
Angaahidi kulipa, ufuwe una kiburi,

Hapendi kusumbuliwa, akonde baki mifupa,
Hapendi kuchukuliwa, mara huko mara hapa, Apenda kufarijiwa,
hali njema kunenepa, Angaahidi kulipa, ufuwe una kiburi.

Maswali

Dhana ya ufuwe imedhihirishwaje katika mashairi haya mawili? (alama 20)

28. Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.

SIWE

1. Siwe ulosema jana, ya kuwa u mashuhuri?

Yakuwa wajuwa sana, haidha huna kiburi
Nchini wajulikana, mwansasasa mahiri
Bungeni tukujiri?

2. Siwe ulotushawishi, kwa chumvi na kwa sukari,

Na matamu matamshi, ukaziteka suduri,
Ukanena penye moshi, moto ndiyo yakwe siri,
Nawe ndiyo hiyo nari?

3. Siwe ulojita moto, uwakao biribiri,

Kamba taita fakuto, litakaoleta kheri,
Utatufunua mato, maisha yawe mazuri,
Tukupe kura waziri?

4. Siwe ulosema hayo, na mengi ukabashiri,
Ukamba wafata nyayo, nyazo ziso utiriri,
Tusiwe na wayawayo, wa kufikirifikiri
Tuachie ujari?
5. Siwe tulokuinua, mabegani kama mwari,
Tungawa twalemelewa, waume tukaasiri,
Kamba tukikuchaguwa, mema kwetu yatajiri,
Tukaketi kusubiri?
6. Siwe ulotugeuka, kwamba leo u waziri,
Wajiona 'melimika, tena ukawa ayari,
Walaghai ukicheka, ukuu umekughuri,
Leo 'mekuwa hodari?
7. Siwe uliyetugura, ukafunga na safari,
Ukaelekea bara, kwa wenzio matajiri,
Ukatuacha majura, na tama kukithiri,
Kanama ushaghairi?
8. Siwe ulojawa raha, za hino yetu sayari,
Ukawa ja vile shaha, hatukupati shauri,
Kutuona ni karaha, wakatiwo twahasiri,
Ushakiya msitari?
9. Siwe uliyetuasi, ukenda pasi kwaheri?
Mbona hutwambii nasi, tukajua yetu shari,
Leo una masidisi, husemi na aso gari,
Ndio mezidi jeuri?
10. Siwe lotwaamgwisho, ukawa wajifakhiri,
Chenye mwanzo kina mwisho, hilo wajuwa dhahiri,
Vyaja kutoka vitisho, kwani hayo si dahari,
Mambo mengi mdawari?
11. Siwe utakayeiza, mwishowe ukithiri,
Siku utayoteleza, kuja kwetu ansari,
Kuja kutubembeleza, kwa nyunga nalo khamri,
'Tanya nazo nadhiri?

Maswali na majibu

(a) Eleza umbo la shairi hili. (alama 4)

- (b) Mwanasiasa anayezungumziwa anatoka pwani au bara? Thibitisha. (alama 2)
- (c) Eleza dhamira na maudhui ya shairi hili. (alama 4)
- (d) Eleza matumizi ya maneno haya kama yalivytumiwa katika shairi. (alama 6)
- (i) Nari
- (ii) Ansari
- (iii) Wakatiwo twahasiri
- (iv) (iv) Ujari
- (v) Ayari
- (vi) Uliyetugura
- (e) Taja na ufanue tamathali ya usemi iliyotawala katika shairi hili. (alama 2)
- (f) Onyesha jinsi mshairi alivyotumia idhini au uhuru wa kishairi: (alama 2)

29. Soma shairi hili kisha ujibu maswali.

1. Mkono inuka, inuka hima, twaa kalamu,
Upate ya'ndika, kwa khati njema, hino mudhumu,
Ipate someka, wenye kusoma, waifahamu.

2. Kuandika anza, anza sikawe, mkono wangu,
Na mimi naanza, nao wajuwe, waja wenzangu,
Wapate jitunza, salama wewe, hawa ndu zangu.

3. Mja sikudhani, sikudhaniya, 'tanigeuka,
Nikaamini, hafikiriya, hatateguka,
Kumbe mwafulani, hakuzoweya, kuaminika,
Nishabaini, ingawa baya, lishanifika.

4. 'Menitenda kisa, kisa adhimu, mja mcheni,
'Mezinduka sasa, n'shafahamu, najuwa kwani,
Ni yangu makosa, najilaumu kumuamini,
Sikuwa napasa, hata sehemu kumuamini.

5. 'Meniuwa mja, mja ni nduli, tahadharini,
Mjaye daraja, nda kikatili, hana imani,
Muonepo mja, kaani mbali, mujitengeni,
Asiye akaja, kwani habali, kuhasirini.

6. Mja hana haya, haya hazimo, mwake usoni,
Mja ni mbaya, hutimba shimo, ungiye ndani,

Na ukisha ngiya, azome zomo, furaha gani,
Mmoja kwa miya, ndiye hayumo, bay a kundini.

Maswali

- (a) Toa anwani ifaayo kwa shairi hili. (alama 2)
- (b) Eleza muundo/umbo la shairi hili (alama 4)
- (c) Kutokana na shairi hili, ni sifa gani ambazo kiumbe (mja) amepewa? (alama 4)

- (d) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari. (alama 4)

- (e) Kwa nini mshairi ametumia ritifaa katika baadhi ya maneno yake? Eleza (alama 2)

- (f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivytumiwa katika shairi hili. (alama 4)
 - (i) Mudhumu
 - (ii) Nduli
 - (iii) Kuhasirini
 - (iv) Hutimba

30. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

MWANAMWARI

1

Ulipokuwa mtoto, u mbichi maungoni,
Sura yenye meremeto, na matiti kifuani, U
kamili wa mkato, u mwari mwenye thamani,
Kumbe vile ni majuto, yalokwandama usoni?

2

Uwendapo kwa miketo, unadunda aridhini,
Damuyo ‘iwile moto, inatembea mwilini,
Na machoyo kutokuto, yanatembea hewani,
Kumbe vile ni masuto, ndio utayobaini?

3

Ulipocheza umeta, kwa nahau na mizani,
Rubaa uliivuta, uli pekeo fanani,
Tamani nikaiteta, kesho itakuwa shani,
Kumbe vile inakuita, siri ilo mafichoni?

4

Mwari usiye matata, ulinipa tumanini,
Na mbele nikaivuta, kaiweka ubavuni,
Nikaota na kuota, usile mwangu machoni,
Mara wageni ‘kateta, wakutie mikononi?

Hata huavunja ungo, wakungwie makuchani,
 Kwa nguvu bila mpango, wakafanya ushetani,
 Midume yenyé mipengo, yenyé tabia ya nyani,
 Wakuhasiri viungo, wakakuacha u duni,
 Ya wapi yangu maringo, na kiburi cha zamani?

Maswali

- (a) Kwa kuzingatia ubeti wa kwanza, taja sifa za anayezungumziwa na mshairi. (alama 3).
- (b) Andika ubeti wa nne kwa lugha ya nathari (alama 5)
- (c) Shairi hili ni la bahari gani? (alama 2)
- (d) Kwa kurejelea ubeti wa mwisho, taja madhila (mateso) yaliyomkumba mwanamwari anayezungumuziwa. (alama 3).
- (e) Taja na utoe mifano ya mbinu za lugha na za sanaa zilizotumika katika shairi hili. (alama 3)
- (f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivytumika katika shairi. (alama 4)
 - (i) Meremeto
 - (ii) Jamala
 - (iii) Fananai
 - (iv) Shani

31. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

ASHA

1. Ewe mama wapendeza, moyo wangu wanikosha,
 Penzi lako naliwaza, roho yangu yachezesha,
Madaha yako yaweza, haribu yangu maisha,
 Mahaba yako punguza, ewe wangu dada Asha.
2. Moyo wangu wanguza, na mawazo wazungusha,
 Viungo vyako vyacheza, *umbile* laburudisha,
 Sura yako yapendeza, wengi wawababaisha
Mahaba yako punguza, ewe wangu dada Asha.
3. Babayo alikuza, pombe zikawalewesha,
 Wifiyo katutawaza, mwili kautelezeshaa,
 Moyowe ukauguza, penzi likavurumisha,
 Mahaba yako punguza, wewe wangu dada Asha.

4. Wengi unawaangaza, mapenzi wawafundisha,
Barabara waongoza, kukufuatia Asha,
Barazani wawalaza, kuni moto waziwasha,
Mahaba yako punguza, ewe wangu dada Asha.

5. *Baragumu* yatangaza, penzi kulisawazisha,
Nipate moyo pooza, matendo kudhihirisha,
Na kuweza tekeleza, mapenzi kuyakanusha,
Mahaba yako punguza, ewe wangu dada Asha.

Maswali

- (a) Eleza muundo wa shairi hili ukizingatia yafuatayo: (alama6)
- (b) Taja mambo ambayo yanamwogofya mshairi. (alama 2)
- (c) Andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari. (alama 4)
- (d) Mwandishi ametumia uhuru wa kishairi katika uandishi wa shairi lake. Taja na utoe mifano. (alama 4)
- (e) Eleza maana ya maneno haya kama yalivytumiwa katika shairi. (alama 4)
- (i) Madaha
(ii) Mahaba
(iii) Umbile
(iv) Baragumu

32. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

GANGA SHINA

1. Maradhi na taathira, ya tego na ulemavu,
Zimeshajiri ishara, za mti kuwa mbovu,
Vitawi kuporapora, mti wazidi ukavu,
Ganga shina la uhai, tanzuze hazigangika.
2. Kutibu si masihhara, kwataka kutuma nguvu,
Na maganga kuyapasa, hata uiache kovu,
Haiji thama nusura, ukichelea mabavu,
Gonga shina la uhai, tanzuze hazigangika.
3. Makongwe yanayokera, yakate kwa maumivu,
Na mizizi ya safura, iliyo mikandamivu, Usiwe nayo
subira, katika utimilivu, Ganga shina la uhai, tanzuze
hazigangika.

4. Rasharasha sio bora, daima iwe rovurovu,
Imwailie imara, hadi isombe kitovu,
Uchome moto sangara, mti uwe muangavu
Ganga shina la uhai, tanzuze hazigangika.
5. Fyekafyeka mipapura, mimea mitatagivu,
Inayonyoya ujira, wa miti mishughulivu,
Nasaha zangu dharura, kesho utakula mbivu
Ganga shina la uhai, tanzuze hazigangika.

Maswali

- (a) Eleza umbo la shairi hili. (alama 4)
- (b) Mwandishi ametumia jazanda katika kuelezea jambo fulani. Taja jazanda hiyo na ueleze maana yake. (alama 4)
- (c) Mwandishi anamaanisha nini anaposema, "Kutibu si masihara kwataka kutumia nguvu"? (alama 2)
- (d) Mwandishi ametumia inkisari. Taja mifano miwili na uiandike inavyotakikana. (alama 2)
- (e) Eleza maana ya kibwagizo cha shairi hili (alama 2) .
- (f) Eleza maana ya msamiati huu kama ulivyotumiwa katika shairi hili (alama 5)
- (i) Kuporapora
 - (ii) Isombe
 - (iii) Sangara
 - (iv) Mipapura
 - (v) Mishughulivu

33. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

- OA MWANA KWETU, OA
1. Oa, sioe anzali, mwenye mwenendo mbovu,
Oa, sioe jamali, wa akili tepetevu,
Oa, sioe jahili, jitu lenye ushupavu,
Oa, muovu sioe, oa mwana kwetu oa.
 2. Oa, akupendezaye, kwa umbile na tabia,
Oa, binti ya babaye, mtambuzi wa sheria,
Oa, mwali ajuaye, vyuoni aloingia,
Oa muovu sioe, oa mwana kwetu oa.

3. Oa, mke kufu yako, mnayefanana hali,
Oa, wa kikozi chako, wa asili na fasili,
Oa, binti, ami yako ikuwiyapo sahali
Oa, muovu sioe, mwana kwetu oa.

4. Oa, mrembo wa shani, mwenye hadhi na murua,
Oa, mwema na watani, uwezapo mgundua,
Oa, sioe muhuni, moto umejipalia
Oa, muovu sioe, oa mwana kwetu oa

5. Oa, mjaze heshima, japo akuzuzukiye,
Oa, muovu sioe, Oa mwana kwetu oa,
Oa, ninakhitimia, mwema ana mwisho mwema,
Oa, muovu tambula, hadi yake ni kuzama.

6. Oa, nakariri oa, kuo a kuna salama,
Oa, muovu sioe, Oa mwana kwetu oa,
Oa, wa macho laini, yaengayo majimaji,
Oa, hwenda yu amini, moyo akakufariji.

7. Oa, khasa mwana ndani, asojua upitaji
Oa, muovu sioe, mwana kwetu oa,
Oa, nakwambia oa, jaribu tena na tena,
Oa, kwa kuangalia na kumuomba Rabana.

8. Oa, upate tulia, na kuepuka fitina,
Oa, muovu sioe, oa mwana kwetu oa,
Oa, imebadilia, dunia yenda kinyume,
Oa, hutaazivika, ukiwa mbora mume.

9. Oa, ninvyoandika, nimtakayo yapime,
Oa, muovu sioe, mwana kwetu oa,
Oa, mtendee mema, mkeo uliyenaye,
Oa, uwe na huruma, roho yake ituliye.

Maswali

- (a) Eleza muundo wa shairi hili. (alama 5)
- (b) Mshairi anamshauri nini mtu atakaye kuo? (alama 8)

(c) Ni mbinu gani ambayo imetawala shairi zima? Itaje na kueleza mbinu hiyo. (alama 3)

(d) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumia katika shairi hili: (alama 4)

- (i) Tepetevu
- (ii) Kufu
- (iii) Hadhi
- (iv) Azirika

34. Soma shairi lifuatato kisha ujibu maswali yanayofuata.

TUNDA

1. Tunda ni kuliangua, chungwa linaloning'nia,
Tunda pia kuchumia, mboga sima towelea,
Jinginelo lipo?
2. Tunda kivuno shambani, lima kisha palilia,
Tunda vinono nyumbani, lima kwa jasho shughulikia,
Jinginelo lipo?
3. Tunda tokeo la kazi, na ujira jipatia,
Tunda matokeo wazi, jitihada jifanyia,
Jinginelo lipo?
4. Tunda pia ni kizazi, wana hao nilozaa,
Tunda tama ya ulezi, wana wataponifaa,
Jinginelo lipo?
5. Tunda letu la uhuru, minyororo jikongoa,
Tunda sote kuwa huru, na mazao furahia
Jinginelo lipo?
6. Tunda ni kwetu uchumi, na chumo kijichumia,
Tunda mwenzangu huchumi, ukaweza kuendelea ,
Jinginelo lipo?
7. Tunda bora utu mwema, yako roho kuilisha,
Tunda la roho nasema, mja kumkamilisha,
Jinginelo lipo?

Maswali

(a) Shairi hili ni la bahari mbalimbali. Zitaje na kuzifafanua. (alama 4)

- (b) Eleza vina na mizani ya beti mbili za mwisho. (alama 3)
- (c) Andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari/ mjazo/ tutumbi. (alama 3)
- (d) Ni mbinu gani ya lugha iliyotumika katika kibwagizo cha shairi hili? (alama 2)
- (e) Toa maana zozote tatu za neno ‘tunda’ kama lilivyotumika katika shairi. (alama 3)
- (f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivytumiwa katika shairi. (alama 3)
- (i) Kuliangua (
 - (ii) Palilia
 - (iii) Kujichumia

35. Soma mashairi yafuatayo kisha ujibu maswali.

‘A’

HOFU YA BINADAMU

1. Hofu zao wanyonge, ni nguvu za matajiri,
Ambazo zinawaponda, wanapotaka usawa,
2. Hofu za watawala, ni kupotoza uhuru,
Wa kutawala kwa mbavu, pamoja na utukufu,
3. Hofu za mwanamke, mwanamke wa sasa,
Ni kutumiwa ja rungu, daima kuwekwa nyuma. 4. Hofu za
mcha – Mungu, ni maisha ya baadaye,
Maana hana hakika, ndio aogopa kifo.
5. Nahofu zao wasomi, ni kwamba wako baidi,
Na wale watetea, ambao si sawa nao.

‘B’

AMANI

- | | |
|---|---|
| 1. Uhuru pia amani
Usifikiri ni zawadi
Ambayo inapeanwa
Pasipo mikwaruzano | 2. Kama wataka hiviyo,
Sharuti uwe tayari,
Kupoteza roho yako
Pamoja na ya mwingine. |
| 3. Uhuru ja ini la faru,
Ambalo kulifikia
Sharti uwe jasiri
Jasiri aso kifani. | |

Maswali

- (a) Linganisha bahari za shairi la ‘A’ na ‘B’. (alama 4)
- (b) i.) Eleza vina na mizani ya ubeti wa kwanza wa shairi ‘A’. (alama 2)
(ii) Vina vya shairi hili vinalielekeza kuchukua mkondo gani? (alama 4)

- (c) Taja na utoe mfano wa mbinu iliyotumika katika ubeti wa mwisho wa shairi la 'B'.
(alama 2)
- (d) Andika ubeti wa pili wa shairi la 'B' kwa lugha ya nathari, (alama 4)
- (e) Andika maneno yafuatayo kwa Kiswahili sanifu kama yalivytumika katika mashairi haya.
(alama 4)
- (i) Nao
- (ii) Ja
- (iii) Aso
- (f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivytumika katika mashairi. (alama 3)
- (i) Utukufu
- (ii) Daima
- (iii) Sharuti

36. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

MKIMBIZI

1. Sikimbii, siogopi, hali yangu nachelea, Sivijui, visa vipi,
pale nyuma kutokea, Niendako, sikuui,mkimbizi
ninaitwa?

2. Sitoroki, nchini mwangu, ugenini kutamani, Sidiriki,
malimwengu, yananizonga jamani, Niendako, sikuui,
usalama nazongea!

3. Siyajui, nisemayo, machafuzi nayapisha, Siyajui,
nionayo, ni maasi ya kutisha, Niendako, sikuui, amani
najitakia.

4. Sipotei, sipumbai, hali njema naisaka,
Sishangai, sitambui, chanzo cha yangu mashaka,
Niendako, sikuui, maskani natafuta.

5. Afrika, Afrika, wana wako tunalia,
Twateseka, twateseka, bara letu kulilia,
Kwa majanga, na visanga, ukimbizi kuzidisha.

6. Viongozi, viongozi, mwongozao Afrika, Mumaizi,
mumaizi, utulivu kuuweka, 'zi nchi zetu, ukimbizi
kupunguza.

Maswali



(a) Lipe kichwa mwafaka shairi hili. (alama 2)

(b) Shairi hili ni la aina gani na kwa nini? (alama 2)

(c) Taja maudhui yanayojitokeza katika shairi hili. (alama 4)

(d) Taja tamathali yoyote ya usemi aliyotumia mshairi na ueleze sababu ya kutumia (alama 2)

(e) Kwa nini mshairi ametumia ritifaa ubeti wa mwisho? (alama 2)

(f) Toa maana ya msamati huu kama ulivytumika katika shairi. (alama 4)

(i)nachelea

(ii)sidiriki

(iii)nazengea

iv)maasi

(g) Andika ubeti wa pili katika lugha ya nathari. (alama 4)

37. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

'SIKATE TAMAA

1. Umeanguka, inuka, simama kama mnazi,

Umechunika, inuka,tia dawa kwa ujuzi,

Sasa inuka, inuka, kijana ianze kazi,

'Sikate tamaa.

2. Usife tamaa, nyanyuka, ni muwoza wa kutenda,

Kuna hadaa, nyanyuka, anza tena kujipinda

Dunia baa, nyanyuka, anza tena kuijunda,

'Sikate tamaa.

3. Sivunje moyo, dunia, ndivyo itakunyanyasa,

Futa kiliyo, dunia, hiyo idhibiti sasa,

Ipe kamiyo, dunia, kamwe siache kufusa,

'Sikate tamaa.

4. Una nguvu, simama, wewe upambane nao,

Una werevu, simama, uziepuke njama zao,

Usiache kovu, simama, ujipunze vumilio,

'Sikate tamaa.

Maswali

(a) Eleza lengo la shairi hili. (alama 1)

(b) Msanii ametumia mtindo gani ili kusisitiza ujumbe wake? Toa mfano mmoja.

(alama 2)

(c) Kulingana na mashairi,tungewezaje kuepuka njama tunazofanyiwa? (alama 3)

(d) Mwandishi anamaanisha nini kwa kusema, 'Usiache kovu'? (alama 2)

(e) Kwa nini mshairi akasema,'Sikate tamaa' badala ya 'usikate tamaa'? (alama 2)

(f) Kuvunjwa moyo kunaleta matokeo gani? (alama 2)

(g) Eleza muundo wa ubeti wa kwanza. (alama 4)

(h) Taja sifa zozote mbili zinazopewa msomaji. (alama 2)

(i) Mshairi asema, 'Umeanguka, umechunika, futa kiliyo.'Mambo haya matatu yanachangia
vipi katika kuendeleza lengo la mshairi? (alama 2)

38. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

1. Mdomo ukiuchonga, kwa maneno ya hadaa,

Na ufundi wenyе kunga, ujuao kuandaa,

Jua umejenga kinga, huonekana wafaa,

Dunia hii ilivyo, neno limekuwa kitu.

2. Viumbe walo wambaji, wabwabwajao maneno,

Hujijengea mtaji, kwa 'yo mingi kikutano,

Jengine hawahitaji, neno kwao tangamano,

Dunia hii ilivyo, neno limekuwa kitu.

3. Watazama wanenaji, wawekao welewano,

Kumbe wana mahitaji, kujipatia vinono,

Jema gani tutaraji, dunia ya mashindano,

Dunia hii ilivyo, neno limekuwa kitu.

4. Yanayosemwa mangapi, maneno yenye mantiki,

Hujui ushike zipi, ahadi za unafiki,

Tahamaki yuko wapi, msema haoneki,

Dunia hii ilivyo, neno limekuwa kitu.

5. Dunia yaelemwa, kwa uongo na uzushi,

Yaenda ikarashiwa, na kumwaiwa marashi,

Kumbe ndani ni shakawa, ninapulizia moshi,

Dunia hii ilivyo, neno limekuwa kitu.

Maswali

- (a) Andika kichwa mwafaka kwa shairi hili. (alama 2)
- (b) Eleza umbo wa shairi hili (alama 4)
- (c) Toa mifano miwili ya kuonyesha jinsi mshairi alivyotumia uhuru wake katika shairi hili. (alama 2)
- (d) Mshairi anatutolea ujumbe gani katika shairi hili? (alama 6)
- (e) Ni kundi lipi la watu ambalo linahusika sana na yanayoendelezwa katika ubeti wa nne? (alama 2)
- (f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyoatumwa katika shairi hili (alama 4)
 - (i) Wambaji
 - (ii) Vinono
 - (iii) Mantiki
 - (iv) Shakawa

39. Soma shairi lifuatato kisha ujibu maswali yanayofuata.

MWAKISU

1. Mwakisu hailaliki, kunguni wameshtadi,
Tena hawamithiliki, waenda wale warudi,
Hung'ata hawashikiki, na muwasho ulozidi, Mwakisu yake
inadi, nahiari tangalachi.
2. Kucha mimi sipepesi, nasongana na jihadi,
Silali ila kiasi, mnadi swala anadi,
Nimeota uyabisi, ukwasu yangu shahidi,
Mwakisu yake inadi, nahiari tangalachi.
3. Si kitanda hicho ndwele, nimechoka nacho hadi,
Kitandwe vipi milele, na mtandaji stadi,
Kukicha tazama chale, mavune na mijeledi,
Mwakisu yake inadi, nahiari tangalachi.
4. Kikazwe kwa madhubuti, shupavu jema jadili,
Siku kenda hazipati, hakina kamwe ahadi,
Hulegea katikati, ni ilaye tangu jadi,
Mwakisu yake inadi, nahiari tangalachi
5. Palipo ngoma ya nini, upatu ni mazidadi,
Keleleze ni za shani, si hapa siyo baidi,



Hupenya masikizini, pasi simile na hadi,
Mwakisu yake inadi, nahiari tangalachi.

6. Nisemapo kwangu kiko, kwalo msikinaidi
Kimenivimbisha viko, kwa mkazo uso budi,
Vilimbili ni viwiko, ganzi tele na baridi,
Mwakisu yake inadi, nahiari tangalachi.
7. Nipatiensi kingine, kitanda bora mufidi,
Malazi yaso mavune, kupata ndiyo muradi,
Nondokane na senene, senene haina sudi,
Mwakisu yake inadi, nahiari tangalachi.

Maswali na majibu

- (a) Zitaje aina nne (4) za dhiki zinazosababishwa na kitanda cha mwakisu kulingana na mshairi. (alama 4)
- (b) 'Uovu wa kitanda cha mwakisu ni mumbile yake'. Jadili kulingana na maoni ya mshairi. (alama 6)
- (c) Uandike ubeti wa pili kwa maandishi ya kinathari. (alama 4)
- (d) Mshairi analinganisha kitanda cha mwakisu na nini? (alama 3)
- (e) Eleza maana ya maneno ayafuatayo kama yalivyotumia katika shairi hili. (alama3)
 - (i) Hung'ata hawashikiki
 - (ii) Mwakisu yake inadi nahiari tangalchi
 - (iii) Malazi yaso mavune, kupata ndio muradi.

40. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

TUKOMBOWE AFRIKA

1. Kitambo tulipoanza, maneno twayatamka,
Kuchapo twazungumza, uhuria twaitaka,
Tukombowe Afrika lakini kipeleleza, hakuna linalotendeka.
2. Tuchunguze ukweli, tuache mbali dhihaka, Kwani
tumeanza mbali, maneno ya kuropoka Sasa tutuze akili,
tuitafiti hakika.
3. Tulijenge tangamano, pamoja kujumuika, Weka hii twa
hino, ala mpya kuzishika, Tuanze maandamano,
mambo yamenifaika.

4. Kaka na dada karani, sasa basi kuandika, Kaamu zote
pipani, mikoba, tai angika, Mushike mashini-gani,
tukombowe Afrika.
5. Wakadhalika dereva, kwa gari unasifika, Tushakusifu u
kileva, wa sukanni kuishika, Mambo ndugu yameiva,
shika kifaru haraka.
6. Si sharuti ya samaki, sukuma pia hulika, Mvivi weka
fataki, mishipi nayo fulka, Twende kutetea
haki, manowari ishafika.
7. Mwanamuziki wa samba, pamwe nasi jumuka, Siku
nyingi umeimba, 'Tukombowe Afrika,' Sasa gita funga
kamba, bunduki jibandika.
8. Kaka mpishi na wewe, kila kuchao wapika, Si kungoja
uambiwe, masufuria finika, Shika japokuwa jiwe, pigania
Afrika.
9. Na tineja muadhamu, vipi unafurahika, Jioni beli-
botomu, bilashi wahuzunika, Hupimi kataamamu, nduyu
zako wateseka.
10. Mwalimu wetu shuleni, kwenye tumeelimika,
Wanafunzi darasani, wafundisha kuandika, Leo watowe
ugani, wafunze zana kushika.
11. Dada yangu mwafulani, mzawa wa Afrika,
Ulitoroka jikoni, uwe 'sawa' nami kaka, Haya toka
ofisini, funga masombo haraka.
12. Poda wacha mumu humu, ya vitani hulipuka,
Jikaze kama ghulamu, Usije ukaanguka, Usawa
ulozuumu, tukombowe Afrika
13. Maneno ulozuumu, tukombowe Afrika, Mwisho ndugu
mshairi, ni sote kujumuka, Tuungane tulo wengi,
tukombowe Afrika.

Maswali na majibu

- (a) Andika kichwa mwafaka kwa shairi hili. (alama 1)
- (b) Ni ujumbe gani unaojitileza katika shairi hili? (alama 2)
- (c) Chambua muundo/ umbo la shairi hili. (alama 4)

- (d) Andika ubeti wa tano kwa lugha ya nathari. (alama 4)
- (e) Onyesha vile mshairi alivyotumia uhuru wake. (alama 4) .
- (f) Andika methali mwafaka kwa shairi hili (alama 2)

41. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Hayawani nondokeya, nondokeya nenda mbali,
Melaniwa huna haya, leo haja kukabili,
Kimbiya nenda Ulaya, upindo wako usuli,
U mbakaji haini.

Watoto waulizani, changudoa mekushinda?
Umezua vyahuni, kuyachafua makinda,
Pinga kama si punguani, adilifu mekushinda,
U mbakaji haini.

Wahanyahanya yayaya, miyaani patupatu,
Matendoyo kubwayaya, umewashinda wenetu,
Kirinyaga na Siaya, kote kote lithubutu,
U mbakaji.

Jogoo kuparagia, kifaranga ni halali?
Ukimwi wawapatia, huna akili kamili,
Nakutungia sheria, takufunga ukubali,
U mbakaji.

Maswali

- (a) Lipe shairi hili anwani mwafaka. (alama 1)
- (b) Shairi hili ni la bahari gani? Thibitisha jibu lako. (alama 4)
- (c) Eleza ujumbe unaojitokeza katika ubeti wa pili. (alama 2)

- (d) Taja na ueleze tamathali tatu za lugha alizotumia mshairi. (alama 3)

- (e) Andika ubeti wanne kwa lugha nathari. (alama 4)

(f) Taja matendo yoyote matatu mabaya yanayosemwa. (alama 3) ◊ Ubakaji/ unajisi.

(g) Eleza jinsi mshairi alivyotumia uhuru wake wa utunzi. (alama 3)

42. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

- | | |
|---|---|
| 1. Wana-haramu,
Hebu nikuulize Mama Afrika,
Kwa nini...
Mimba changu ukajichukulia,
Ya haramu sana ilotepetea, | 2. Ukazaa wana walojahila,
Wasiojijua, wala yao njia?
Kuzurura ukamalizika,
Bila muruwa, heba kukupotea,
Ukawa ganda la kupita njia. |
| 3. Usiye maoni ya kuonelea?
Kwa nini...
Ukazaa kizazi kilo kiwete,
Kilohasirika kwa wakati wote,
Kilichopagawa kwa wingi kite,
Hata utu wake ukakipotea? | 4. Ah moyo waumia!
Hupigwa na mshangao,
Niwfikiriapo,
Wale barobaro wanao,
Wasaliti wanati wale na vyeo,
Walomdhiki mama mzazi wao,
Kwa muradi wao. |
| 5. Lakini sijali,
Sijali kwani najua,
Siku moja itawadia,
Wana-haramu watajuhalalia,
Kila cha haramu kukuondolea,
Na kukutakasa. Mama wasikia? | 6. Mama wasikia?
Hivyo siku itakapfika,
Kila dhulumu litajikatika,
Na kila mahali utadhihirika,
Mwisho wa salata na uharamia. |

Maswali na majibu

- (a) Shairi hili ni la bahari gani? (alama 2)
- (b) Mwandishi analalamikia mambo yapi katika shairi? (alama 6)
- (c) Mwandishi ametumia mbinu gani katika kutumia maneno “Mama Afrika”? Kifungu hiki kimetumika kumaanisha nini? (alama 2).
- (d) Andika ubeti wa nne kwa lugha ya nathari. (alama 4)
- (e) Mtunzi ana maana gani anaposema, “ukazaa kizazi kilo kiwete”? (alama 2)
- (f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi. (alama 4)
- (i) Murua
- (ii) Kite
- (iii) Kukutakasa
- (iv) Salata

43. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

KIZA

1. Kiza ni mwambo wadhila, pulika unisikiye,
Kiza kinapotawala, hasara itukutiye,
Kiza kiumbe humla, kipande asibakiye,
Kiza ukosapo hila, ni lazima kikugwiye,
2. Kiza ni ghubiko, usiku lituvamiye,
Kiza hupamba mwili, waovu washangiriye,
Kiza huja mahali, vibandani waingiye,
Kiza nafuzi katili, yafaa tuikimbiye.
3. Kiza lifungapo wingu, na dharuba ituliye,
Kiza mfano wa pingu, humfunga atakaye,
Kiza chini ya myungu, twaihofu hatariye,
Kiza hakiishi mizungu, hadi robo kiitwaye.
4. Kiza ujapo ukame, kiu itushikiliye,
Kiza viro vitufume, uhai usisaliye,
Kiza kijapo kinyume, pengine usidhaniye,
Kiza kweli mwanamume, ndani mwake usingiye.
5. Kiza tetema aridhi, zilizala niwambiyiye,
Kiza maafa huhodhi, viumbwe yawajiliye,
Kiza mangapi maudhi, sitotowa hesabuye,
Kiza mwenzangu siridhi, kila siku kiambaye.
6. Kiza yajiri maradhi, mwache kiumbe aliye,
Kiza kuishi huridhi, watamani ujifiye,
Kiza itimu faradhi, nduli akufahamiye,
Kiza ndugu kumradhi, mwepuke simvamiye.

Maswali na majibu

- (a) Eleza kiza kwa mujibu wa mshairi (alama 2)
- (b) Fafanua hasara zinazosababishwa na kiza. (alama 4)

(c) Mshairi alikuwa na lengo gani alipotunga shairi hili? (alama 2)

(d) Eleza umbo la shairi hili. (alama 6)

(e) Andika ubeti wa sita kwa lugha ya nathari. (alama 4)

(f) Toa maana ya mishororo ifuatayo: (alama 2)

(i) Kiza ni kiwambo wa dhila, pulika unisikiye.

(ii)Kiza hupamba mwili, waovu washangiria.

44. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

UKOLONI NA UKOLONI MAMBOLEO

1

UKOLONI: Naijusha, nakuacha utawale

Nakupisha, sina haja ya kelele

Zimekwisha, zama zangu ni za kale

Naondoka.

2

UKOLONI MAMBOLEO: Nipe njia, nikuonyeshe kilenge

Naingia, nilieneze varange

Nipe njia.

3

UKOLONI: Najikosha, mimi nilokataliwa

Najepusha, sitaki kulaumiwa

Sepotosha, nilifunza ya muruwa

Naondoka.

4

UKOLONI MAMBOLEO: Nasikia, lijitia imani

Kawachia, ati wawe furahani,

Yangu nia, wote wawe mashakani

Nipe njia.

5

UKOLONI: Waliona, niliyyoyatenda mabaya

Kupendana, wao walishikiliya

Wakatuna, uhuru kunyang'anyia

Naondoka.

6

UKOLONI MAMBOLEO: Nitazuwa, ujanja uliokithiri

Watakuwa, wachachawa kufikiri

Na muruwa, wao wataughairi

Nipe njia.

7

UKOLONI: Walalame, watangaze kwa kiburi

Na waseme, sikuwamwaia heri
Ni kinyume, mimi naaga kwaheri
Naondoka.

8

UKOLONI MAMBOLEO: Wajuaje? Wanaadamu thakili
Watendeje, wazimu kwao akili
Waningoje, niwatie mushkili
Nipe njia.

9

UKOLONI: Kwa mapana, nakupa njia upite
Choyo sina, ila nimengia kite
Kwa bayana, mwishowe waje wajute
Naondoka.

Maswali

- (a) Shairi hili laweza kuwekwa katika bahari mbili tofauti. Zitaje na ueleze sababu.
(alamu 2)
- (b) Yaeleze maudhui ya shairi hili. (alamu 4)
- (c) Eleza matumizi ya majazi katika shairi hili. (alamu 4)
- (d) Eleza sifa za Ukoloni na Ukoloni Mamboleo. (alamu 4)

- (e) Kwa nini mshairi anarudiarudia maneno yafuatayo: (alamu 2)
 - (i) Naondoka
 - (ii) Nipe njia.

- (f) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha ya nathari. (alamu 4)

Maswali ya ziada

- (a) Eleza muundo wa shairi hili. (alamu 4)
- (b) Nafsineni katika shairi hili anasema na pande mbili. Zieleze pande hizo. (alamu 4)
- (c) Eleza matumizi ya majazi katika shairi hili. (alamu 2)
- (d) Bainisha toni la shairi hili. (alamu 2)

- (e) Eleza umuhimu wa viishio vya beti za shairi hili. (alamu 4)

45. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

1. Hisani inanyunuza,

2. Hisani na ukarimu,

Mdogo ikamkuza,
Kinda itamkuza,
Hisani ikamlea.

Hadi ni vitu muhimu,
Mfanowe mlizamu
Hisani kufadhiliwa.

3. Hisani kama johari,
Haipati mjasiri,
Ni joho lenye fahari,
Hisani ukitumia.

4. Basi sikia watoto,
Hisani ni jambo zito,
Si pesi kama kokoto,
Si kitu cha kubeua.

5. Hisani yaweza kupa,
Utajiri kukukopa,
Ukaweza kunenepa,
Lafidhi njema kutoa.

6. Ihsani haiodzi,
Mfano kama mizizi,
Zaidi ya utoshezi,
Unapoitumilia.

7. Hisani ni kama fimbo,
Husotea hata ng'ambo,
Ikawavuta warembo,
Hisani bila udhia.

8. Hisani njema huweka,
Ni akibayo ya myaka,
Japo wito kiitika,
Hisani itasalia.

9. Basi dunia si fosi,
Yataka mwendo wa ngisi,
Wawapi kina Msosi,
Nguvu walikitumia.

10. Ikupe mema makazi,
Wewe na wako uzazi,
Iwe kama simulizi,
Na wana wakitumia.

11. Nanyi ndugu fikirini,
Muikumbuke hisani,
Haiodzi ihisani,
Daima huchipukia.

12. Hisani yanipa sifa,
Yanongeza maarifa,
Na hata kama nikifa,
Wanangu watatumia

13. Watatumia maisha,
Hisani nilobakisha,
Hadi mwisho wa maisha,
Na kuondoka dunia.

14. Najua mtakubali,
Haya bila shikeli,
Asiyejua fadhili,
Nyama kasoro mkia.

Maswali

- (a) Fafanua arudhi zilizotumiwa kutunga shairi hili. (alama 4).
- (b) Kina kinachokaririwa sana katika shairi hili huitwaje? (alama 1)

- (c) Shairi hili huitwaje? (alama 1)

- (d) Ukierejelea shairi hili, fafanua sifa za mashairi ya aina hii. (alama 4) .

- (e) Ni upi ujumbe wa mshairi? Toa mifano minne. (alama 4)
- (f) Taja na ufafanue mifano minne ya matumizi ya lugha katika shairi. (alama 4)
- (g) Linganisha na kutofautisha maneno 'Hisani na lhisani.' (alama 1)
- (h) Taja mstari unaolingana kimaana na *Japo wito kiitika*.

46. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

1. Piteni jamani piteni, piteni haraka,
Nendeni, nendeni huko mwendako,
Mimi haraka, haraka sina,
Mzigo wangu, mzigo mzito mno,
Na chini sitaki kuuweka.

2. Vijana, kwa nini hampiti,
Kwa nini mwanicheka,
Mzigo nilioubeba haupo kichwani,
Lakini umenipinda mgongo na miguu,
Na lazima nijiegemeze, kichwa chini nendako.

3. Haya piteni! Piteni haraka! Heei!
Mwafikiri mwaniacha nyuma !
Njia ya maisha ni moja tu,
Huko mwendako ndiko nilikotoka,
Na nilipofika wengi wenu hawatafika.

4. Kula nimekula na sasa mwasema,
Niko nyuma ya wakati,
Lakini kama mungepita mbele,
Na uso wangu kuutazama,
Ningewaambia siri ya miaka mingi.

Maswali

- (a) Ni mzigo gani unaozungumziwa katika shairi? Thibitisha. (alama 3)
- (b) Toa ujumbe unaodokezwa kutokana na mafungu yafuatayo:
- (i) Njia ya maisha ni moja tu. (alama 1)
- (ii) Kwa nini mwanicheka kisogo? (alama 1)

- (c) Mwandishi anasema kuwa anaweza kuwaambia vijana siri ya miaka mingei. Hii ni siri gani? (alama 3)
- (d) Thibitisha kuwa utunzi huu unaweza kuchukuliwa kuwa ni shairi. (alama 6)
- (e) Pendekenza methali zozote mbili zinazodokezwa katika utunzi huu. (alama 2)
- (f) Taja na kutolea mifano mbinu zozote mbili za lugha katika shairi hili. (alama 2)

47. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

1. Jicho, tavumiliaje, kwa hayo uyaonayo?
Kicho, utasubirije, maonevu yapitayo,
Kwacho, lijalo, nimechoka vumiliyo,
Naandika!

2. Moyo, unao timbuko, maudhi tuyasikiayo,
Nayo, visa na mauko, wanyonge wayakutayo,
Kwayo, sina zuilikio, natoa niyahisiyo,
Naandika!

3. Hawa, wanatumiliya, dhiki wavumiliayo,
Hawa, mamiya mamiya, na mali wazalishayo,
Hawa, ndo wanaoumiya, na maafa wakutayo,
Naandika!

4. Hawa, sioni wengine, kwao liko angamiyo,
Hawa, uwapa unene, watukufu wenye nayo,
Hawa, bado ni wavune, kwa shida waikutayo,
Naandika!

5. Bado, wawapo mabwana, wenye pupa na kamiyo,
Bado, tofauti sana, kwa pato na mengineyo,
Bado, tuling'owe shina, ulaji na pia choyo,
Naandika!

Maswali

- (a) Shairi hili laweza kuwekwa katika bahari tatu. Taja na kueleza. (alama 3)

- (b) Eleza dhamira ya mshairi. (alama 2).
(c) Onyesha mifano miwili ya uhuru wa kishairi kama ilivyotumika katika shairi. (alama2) .
(d) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari. (alama 4)

- (e) Tambulisha kwa kutolea mifano mbinu zozote tatu za sanaa. (alama3)
(f) Fafanua sifa za kiarudhi katika ubeti wa tano. (alama 3)

- (g) Eleza maana ya maneno yafutayo kama yalivyotumika katika shairi. (alama 3)
(i) Zuilikio
(ii) Wavune
(iii) Wenye pupa na kamiyo

48. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

TOHARA KWA WANAWAKE

1. Tohara, kwa mwanamke, ni hatari,
Madhara, kwa wake uke, hushamiri,
Hasara, ya peke yake, hudhihiri,
Zinduka!

2. Epuka, hao ngariba, wajuaji,
Hufika, navyo viroba, wachinjaji,
Kumbuka, hawana tiba, wauaji,
Zinduka!

3. Kiwembe, kilochafuka, na kibutu,
Viumbe, huathirika, ni kwa kutu,
Siombe, yakakufika, mwana kwetu,
Zinduka!

4. Maradhi, hujitokeza, ya vidonda,
Yaridhi, kujichomoza, pepopunda,
Na hedhi, hukuchagiza, ikavunda,
Zinduka!

5. Isiwe, wembe mmoja, wengi wari,
Ujuwe, UKIMWI huja, ni hatari,
Na iwe, katu si hoja, kuwa mwari,
Zinduka!

6. Mzazi, kujifunguwa, idhilali,
Huwezi, kujitanuwa, ni muhali,

Ni wazi, husumbuliwa, na misuli,
Zinduka!

7. Wacheni, mila dhaifu, zinatesa,
Kwepeni, amali chafu, na waasa,
Shikeni, uadilifu, tangu sasa,
Zinduka!

Maswali

- (a) Kwa mujibu wa mshairi, tohara kwa wanawake inastahili kupigwa marufuku.
Fafanua. (alama 2)
- (b) Taja magonjwa matatu yanayosababishwa na tohara kwa wanawake. (alama 3)
- (c) Eleza ujumbe unaojitokeza katika ubeti wa saba. (alama 1)
- (d) Toa neno moja lenye maana sawa na *tohara kwa wanawake*. (alama 1)
- (e) Fafanua maana ya mishororo ifuatayo : (alama 2)
- (f) Eleza sifa za ngariba kulingana na mshairi. (alama 1)
- (g) Eleza maana ya maneno yafuatayo :
 - (i) Kibutu
 - (ii) Ikavunda
 - (iii) Wari
 - (iv) Muhalii
 - (v) Amali

49. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

1.Una moyo gani, n'nakuuliza, wangu *muhisan?* Na kiasi
gani, unavyojiweza, ijapo tufani?

Ukiwa laini, utajipoteza, usijibaini, Kusimama pweke
kwataka makini.

2.Zitavuma pepo, zitakupuliza, uanguke chini, Ela uwe papo,
unajikweleza, na kujiamini, Utikishapo, umejiumiza, pigo la
moyoni, Kusimama pweke kwataka makini.

3.Utie *migati*, ya kukuoteza, hapo aridhini, Kwa nia ya dhati,
usiogeza, au kubuni
Zidate baruti, uwe wapuuza, weleke sokoni, Kusimama

4.Sishike vishindo, na mauzauza, ya *kukuzaini*, Kita kama nyundo, ukiniuliza, unayoamini, Na uje mkondo, *utadidimiza*, kujipa mizani, Kusimama pweke kwataka makini.

5.Wengine wasiwe, unaoweleta, yaliyo maanani, Wewe ndiwe, utawafeuza, pindipo mwakani, Ela jichukuwe, pia kujikaza, katika midani, Kusimama pweke kwataka makini.

Maswali

- (a) Eleza umbo la shairi hili. (alama 2)
- (b) Ukizingatia shairi ulilopewa, eleza jinsi mtunzi alivyotumia uhuru wake. (alama 6) .
- (c) Ni ujumbe gani unaotolewa na mshairi kwa wasomaji wake? (alama 2) .
- (d) Kibwagizo cha shairi hili kina maana gani? (alama 2)
- (e) Eleza mbinu za lugha zilizotumika katika ubeti wa kwanza wa shairi. (alama 3)
- (f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivytumika katika shairi. (alama 5)
- (i) Muhisani
 - (ii) Migati
 - (iii) Kuihuni
 - IV) Utadidimiz
 - v) Kukuzaini

50. Soma mashairi yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.

SHAIRI 'A'

1

Baba panga walinoa, makali kutia,
Nini kigumu zidia, wataka katia,
wajisemea, mori kuzidia,
Baba naogopa!

3

Moyoni wajiwazia, kichwa kutikisa,

2

Baba kionya hiyo, mikunjo pajini,
Tabasamu uli nayo, haipo usoni, Pekeo
Inaogofya surayo, mtima kugusa, Baba naogopa!

4

Baba unatufungia, nyumbani mo kweli,

Jambo gani fikiria, mtima kugusa,
kipangua, moyo kukuasa,
naogopa!

Panga linatishia, lilo na makali, Unapanga
Baba nini yako nia, jibu langu swali, Baba
Baba naogopa!

5

Baba mwili wakucheza, meno kakenua,
Mboni nyekundu tuliza, kaka kakazia,
Baba sichoki kuliza, niayo nambia,
naogopa!

7

A! Baba kaka kafyeka, umeshamuwa!
Kakukoseani kaka, huruma nonea,
mwingine umeshika,
Baba meshaua!
Baba situuwe!

9

Baba na watu watatu naye, wanao damuyo,
Ona kijito damuye, wapi imaniyo?
usiyé, katili wa moyo,
Baba waniua!

6

Baba kiwa lazima, kutaka tuuwa,
Tufukuze tu wazima, Mola hurumia,
Tungawa hatuna mama, mja saidia, Baba
Tuna haki kwishi!

8

Masikini ndugu zangu, njooni tukimbie,
Shikeni kiganja change, mbali kimbilie, Na
Mili yenu ole wangu, barafu fanoe, Hata naye piya?

10

Baba wanijia pia, name kumaliza,
Wa nini ultuzaa, bila ya kuwaza, Jiwe huruma
Na kifo huhitimia, bila kukuza soweza, Baba situuwe!

SHAIRI 'B'

1. Pindi ilipomjia, khabari za binti kazaliwa,
Uso ulimsawijika, kwa soni akachanganyikiwa,
“Hii ni nukhusi?
Aka, ni nakama!
La, ni neema!
Bali si beluwa?”
Wapi uso aufiche?
auzike?
Ya kuzaliwa ‘mke’.

2. Nitawatolea kisa...
Nawatangulizia sasa,
Kisa kilichoanza,
Kinachoendelea hasa,
Hakijawahí kukoma,
Baharini wala bara,
Kote kimeenea, Au mchangani
Namna wanavyomtesa. Izara hii asiipate!

3. Kiumbe dhalili wamemfanya,
Lini atathaminiwa?
Kisa chenyewe kitendawili,
Mwenye busara atoe taawili,
Ya haya mambo mawili,
Maisha bila ‘mke’ ni awali,

Kisa kingeendelea?
Lulu iliyohifadhiwa ni la pili,
Kisa kingeendelea?

Maswali

- (a) Lipe shairi la 'A' kichwa mwafaka. (alama 2) B
- (b) Eleza dhamira ya : (alama 2)
- (i) Shairi la 'A'
- (ii) Shairi la 'B'
- (c) Taja arudhi za shairi 'A'. (alama 4)
- (d) Fafanua ujumbe wa shairi la 'B'. (alama 2)
- (e) Shairi la 'A' ni la bahari gani? Thibitisha jibu lako. (alama 2) .
- (f) Andika ubeti wa saba wa shairi la 'A' katika lugha ya nathari. (alama 4)





Strive for progress

The following materials are also available;

- 👉 High school topical questions
- 👉 Primary topical questions
- 👉 High school summarised notes
- 👉 KCSE & KCPE predictions
- 👉 Termly exams
- 👉 Updated schemes of work
- 👉 Highschool mocks and pre-mocks
- 👉 KCPE & KCSE past papers
- 👉 Setbook questions and guides

N/b, all questions are free but notes and set guides incl

welcome for topligt publishers products

Call/text/WhatsApp Sir Abraham@0729125181

03 December 2021